

**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR**

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6. Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed - MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo - MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma - MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali - MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume - MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma - MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/ Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed - MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico - MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib - MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib - MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said - MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim - Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman - Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri - Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum - Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis - Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla - Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma - Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo - Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar - Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopopo
47. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahaman Masoud	-	Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali-	-	Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Fom Mussa	-	Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini -	-	Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy-	-	Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nane – Tarehe 30 Septemba, 2016

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Shehe Hamad Mattar) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ushahidi Sura ya Tano na Kuandika Sheria Mpya ya Ushahidi na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Namba 2 ya Mwaka 2015, Kuweka Masharti Bora Zaidi, kwa ajili ya ufanisi na usimamizi imara wa Mfuko na mambo yanayohusiana na hayo. Kusomwa kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kutunga Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma kwa Kuweka Masharti Bora ya Kudhibiti na Kusimamia Fedha za Umma na kuweka mambo mengine yanayohusiana na hayo na Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Serikali Namba 12 ya Mwaka 2005. Kusomwa kwa Mara ya Kwanza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uzaji wa Mali za Serikali Namba 9 ya Mwaka 2005 na Kutungwa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na Uzaji wa Mali za Umma na Kuweka Masharti mengine yanayohusiana na hayo. Kusomwa kwa Mara ya Kwanza. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hoja ya Mjumbe kuhusu maombi ya wananchi ya kutaka hatua za serikali kuhusu upatikanaji wa huduma za afya katika Taasisi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kuweka mezani Hoja ya kuhusu Ukiukwaji wa Sheria kwa baadhi ya

Taasisi ambazo zinatakiwa kuwasilisha taarifa zake mbele ya Baraza lako tukufu kwa mujibu wa Sheria. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (Makofi)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kulingana na *order paper* ya leo kuna mabadiliko madogo kwa dharura na badala ya kuita Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais nitampa nafasi Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kujibu maswali yake.

Waheshimiwa Wajumbe, nadhani tumekubaliana hilo.

Wajumbe: Ndio.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 190

Ruhusa za Ufanyaji wa Biashara za Mitaani kwa Vijana

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi amesema, vijana wanaofanya biashara mitaani hawastahili kubugudhiwa, ili wapate riziki na kufanikisha utekelezaji wa ilani ya CCM ya vijana kujiajiri, ili kuondokana na umasikini.

- (a) Je, Zanzibar tumejifundisha nini juu ya uamuzi wa Rais John Pombe Magufuli, kwa kuwajengea wafanyabiashara wadogo wadogo (Machinga) eneo la Kariakoo kuendelea na biashara zao bila ya kubugudhiwa.
- (b) Je, ni lini serikali itaachia wafanye biashara zao katika maeneo ya Darajani, Mchangani na maeneo ya katikati ya Mji Mkongwe.
- (c) Je, hatua ya kuwakamata wafanyabiashara wadogo wadogo wakiwemo wauza kahawa, mikate, njugu, machungwa, magazeti inawasaidia kupunguza umasikini au kuzidisha umasikini na uhalifu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 190 lenye vifungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- a) Baraza la Manispaa limejifunza kutokana na uamuzi wa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwamba, wafanyabiashara wadogo wadogo ni wahusika wengine katika uendelezaji wa Miji. Kwa hiyo, Mabaraza ya Miji yana wajibu wa kuwatengea sehemu maalumu kwa ajili ya kuendelea na biashara zao bila ya kughudhiwa, kwa mujibu wa sheria na kanuni ambazo zimetungwa, ili kutunza mazingira mazuri ya Mji.
- b) Serikali itaachia wafanyabiashara katika maeneo ya Darajani, Mchangani na maeneo mengine ya Mji Mkongwe baada ya kukamilika na kutekelezeka mpango wa Uendelezaji Ukanda wa Darajani (Darajani *corridor*), ili wafanye biashara katika maeneo yaliyopangwa kwa mujibu wa sheria na si barabarani, kwa ajili ya utunzaji na usafi wa Mji na mazingira endelevu katika Mji.
- c) Hatua ya kuwakamata wafanyabiashara wadogo wadogo imesaidia kuweka nidhamu na haiba ya Mji, pia itasaidia kupunguza umasikini kwa vile wafanyabiashara hao wamepangiwa sehemu maalumu ambayo itapelekea kukusanya mapato kwa mpangilio mzuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Waziri. Lakini nataka kumwambia Mhe. Waziri, kwamba serikali hii isingekuwepo madarakani bila ya kuwepo wananchi, kwani wananchi ndio serikali.

Serikali imefanya vikao vingapi na wafanyabiashara wadogo wadogo, kwa ajili ya kujua matatizo ambayo wanayo ikiwemo kukamatwa na wengine kupoteza mitaji yao na hata wengine kunyolewa vipara bila ya ridhaa yao. Kwa kuwa vijana ndio nguvu kazi na wanahitaji kukopesheka, na serikali imekuwa ikisema tu kwamba tuna huruma kwa mdomo lakini kwa vitendo hatuoni.

Kwa hivyo, ni lini serikali itakaa na wafanyabiashara wadogo kwa ajili ya kuwapa mitaji na kuweza kuwakopesha na wakaweza kukopesheka mabenki.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti,

- (a) Serikali inatambua kwamba kuwepo kwake madarakani kunatokana na kuwekwa na wananchi hasa Serikali ya CCM. Lakini Serikali hiyo ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, katiba na utawala bora. Kwa kweli bila ya kufuata misingi ya sheria na utawala bora, basi nchi yoyote inaweza ikatokea fujo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wafanyabiashara wadogo wadogo wamekuwa wakielimishwa mara kadhaa na Baraza la Manispaa juu ya kufanya biashara kwa kufuata sheria.

Vile vile, kama nilivyojibu swali mama kwamba sisi tunatambua mchango mkubwa wa wafanyabiashara wadogo wadogo na ndio maana baada ya kuwaondosha katika maeneo yasiyoruhusiwa kisheria, basi tumewatengea eneo la Saateni, ili waende wakajipatie riziki zao ambazo ni halali.

- (b) Serikali inawajengea vipi mazingira wafanyabiashara. Kwa kweli, serikali imeweka kisheria Mfuko wa Uwezesaji na imetoa fursa kwa Mabenki ya Biashara kwa kuwawezesha wananchi wa Zanzibar hasa wafanyabiashara wadogo wadogo kwenda kufuata utaratibu, kwa ajili ya kuchukua mikopo katika Mabenki ya Kibiashara na katika Mifuko mbalimbali ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeiweka, kwa lengo la kuweza kujiendesha maisha yao pamoja na familia zao. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia wimbi kubwa la vijana wetu ambao kwa asilimia kubwa wamekata tamaa kwa kukosa maeneo ya kufanyia biashara zao, na kwa kuzingatia Mfuko wa Kusaidia Vijana na Akinamama kuwawezesha kufanya ajira fedha zipo na zinapatikana, lakini maeneo yanakosekana.

Je, Mhe. Waziri tukiachia maeneo ya miji, lakini katika baadhi ya majimbo kuna maeneo mazuri kama wizara itakuwa imejipanga vizuri kuwajengea angalau maeneo kwa ajili ya kufanya biashara zao. Kwa hivyo, wizara ina mpango gani wa kupata nafasi katika maeneo hayo au kama viongozi wa majimbo wanayo kuyatoa, ili wajengewe na wapate kufanya biashara zao katika hali ya uhalali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nakiri kwamba maeneo yaliyotengwa na serikali, kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo ni machache. Hata hivyo, wafanyabiashara wadogo wadogo wana wajibu na jukumu la kutafuta maeneo katika maeneo ya watu binafsi, ili kufanya biashara zao.

Lakini serikali inao mpango mkubwa sana wa kuweza kujenga maeneo maalumu ya biashara kama nilivyosema. Kwa mfano, Darajani katika majengo manne yatakayojengwa, basi lipo jengo maalumu kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo. (*Makofi*)

Katika eneo la Michenzani patakapojengwa *Shopping Mall* nyengine, basi lipo jengo maalumu kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo. Kwa maana hiyo, serikali itaendelea kupanga maeneo maalumu ya kufanyia biashara, na katika kila eneo la kufanyia biashara litakalotengwa na serikali, basi litatengwa eneo maalumu kwa ajili ya wanyabiashara wadogo wadogo pamoja na wale wakubwa. (*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza napenda niipongeze serikali kwa kuondosha wananchi pale wanaofanya kazi, ili kuweka mazingira safi na kujenga hali iliyokuwa nzuri pamoja na kuwapatia sehemu ya Saateni kwa muda au kudumu.

Swali langu ni moja ambalo litakuwa na vipengele (a) na (b).

Kwa kuwa wananchi walioondoshwa pale maeneo ya Darajani ni wengi na watazidi kuongezeka, nchi yetu ni ndogo na sehemu waliopatiwa Saateni sio kubwa ya kutosheleza.

- (a) Je, ni lini au wizara imefikiria vipi kuhakikisha kwamba lile eneo la Saateni watajengewa jengo la ghorofa, ili watu waenee wengi na wasije wakajaa na halafu likawa eneo dogo kwa muda mfupi.
- (b) Katika sehemu ya Saateni kuna maduka yamejengwa, hivi ni nani aliyetoa ruhusa pale ya kujenga yale maduka, kwa sababu yamechukua nafasi wala hayako katika mipango mizuri kwenye maeneo yale. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf Jusab swali lake. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, watu wengi wanashangaa kwa nini nalitaja hili jina la Jusab. Kwa kweli, Mhe. Abdulatif alikuwa ni miongoni mwa mwakilishi mwenzetu katika Baraza hili kwa hiyo moto huzaa moto. (*Kicheko/Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa katika eneo la Saateni utaratibu uliotumika mwanzo haukuwa utaratibu mzuri wa kuwapa baadhi ya wafanyabiashara binafsi kujenga maduka. Kwa hivyo, utaratibu huo sasa serikali kupitia Baraza la Manispaa tunaupitia upya na maeneo tunayoyajenga sasa yanajengwa na serikali kupitia Baraza la Manispaa, ili kuhakikisha kwamba udhibiti na kutoa nafasi sawa kwa wafanyabiashara wenye mahitaji ya kufanya biashara yanapatikana.

Vile vile, kwa kuwa eneo la Saateni ni eneo la muda na pale tu tutakapoamua kulijenga eneo la Saateni iwapo itakuwepo nafasi ya kuweza kujenga eneo la wafanyabiashara wadogo wadogo, basi tutazingatia suala la kulipanga vizuri kama tulivyoanza hivi sasa.

- (b) Je, eneo hilo hatuna mpango wa kujenga ghorofa. Mhe. Mwenyekiti, eneo hili kwa sababu ni la muda, bado serikali imetoa eneo hili ni *temporary*, yaani la muda. Kwa hivyo, pale tutakapoamua serikali kwamba eneo hili nalo lijumuishwe katika maeneo ya biashara hasa wafanyabiashara wadogo wadogo, basi maoni yake Mhe. Mwakilishi tutazingatia na huko ndiko tunakoelekea hivi sasa.

Nam. 159

Kujaa kwa Eneo la Kuzikia la Mwanakwerekwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Eneo la kuzikia (makaburi) la Mwanakwerekwe kwa miaka mingi limekuwa likitumika kuzika wafu na hadi kufikiriwa kuwa limeshajaa. Hivi sasa kumekuwa na mtindo wa kuyajengea makaburi hayo na kupelekea nafasi ya kuzikia kuzidi kuwa ndogo.

- a) Je, serikali ina mpango gani wa kuweka alama za kudumu katika makaburi hayo, ambazo zitachukua nafasi ndogo kuliko ilivyo hivi sasa.
- b) Kwa kuwa eneo la Mwanakwerekwe limeshaonekana kujaa na nafasi iliyobakia kuwa ni ndogo sana. Je, serikali imeshatafuta eneo jengine la kuzikia na kulifunga eneo la Mwanakwerekwe.
- c) Hatua gani zinachukuliwa kudhibiti vitendo vya uharibifu wa mazingira ya eneo la makaburi ya Mwanakwerekwe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 159 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ofisi yangu kwa kushirikiana na taasisi husika inaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya kutoyajengea makaburi, kwani kufanya hivyo kunapelekea kufinya nafasi na badala yake wayaweke alama ambazo hazitachukua nafasi kubwa.

(b) Ni kweli kwamba eneo la makaburi ya Mwanakwerekwe linakaribia kujaa na imebakia nafasi ndogo sana. Kwa kuzingatia umuhimu wa kutatua changamoto hiyo, serikali tayari imeshatenga eneo jengine mbadala liliopo Kama, Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja walipozikwa baadhi ya wenzetu waliofariki katika ajali ya Meli ya *MV. Spice Islander*.

(c) Baraza la Manispaa ya Magharibi 'B' linatambua kadhia ya uharibifu wa mazingira katika maeneo ya Mwanakwerekwe makaburini na hatua mbali mbali zinaendelea kuchukuliwa na zimechukuliwa kudhibiti kadhia hiyo zikiwemo:

(i) Kufanya mikutano na jamii inayozunguka eneo hilo na kuwaelezea athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira.

(ii) Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kuwakamata wanaochimba mchanga katika eneo hilo.

(iii) Kuwaruhusu wahisani kujenga ukuta kuzunguka makaburi hayo.

(iv) Kupiga marufuku magari ya ng'ombe na punda katika maeneo hayo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kutangaza eneo, je, ni lini eneo jipya litatangazwa rasmi na serikali ili wananchi wapate kulitumia na kujua sio kulitangaza hapa tu.

Pili, tatizo la uchimbaji mchanga limeathiri makaburi mengi yakiwemo ya Waislamu na Wakristo. Hata hivi sasa kaburi la Mwanaharakati wa Mapinduzi Mhe. Brg. Adam Mwananjuki limo katika hatari ya kutoweka. Kuna sababu

gani ikiwa wewe ni Mhe. Waziri una vikosi vingi tu, Darajani umeweza kudhibiti kulinda kwa nini kule kusilindwe. Hebu waeleze wananchi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, bado eneo la makaburi la Mwanakwerekwe halijajaa kabisa. Hata hivyo, serikali iliamua kutenga eneo la Kama kama nilivyojibu swali langu mama kutokana na vile vifo vya Meli ya *MV. Spice Islander*. Tulianza kulitumia eneo lile kama ni eneo la dharura, na kwa sababu serikali tumeliona ni eneo muafaka badala ya Mwanakwerekwe muda utakapofika serikali italitangaza eneo lile kama ni eneo rasmi sasa la makaburi kama lilivyotangazwa lile la Mwanakwerekwe.

Pili, nimeweza kutumia vikosi kuwaondosha wafanyabiashara wadogo wadogo katika eneo la Darajani. Nimefanya vile baada ya wahusika kutofuata sheria bila shuruti, kwanza ieleweke hivyo. Nikiwa waziri ninayeshughulikia masuala ya idara maalum na serikali kwa jumla hatukurupuki tu, kutumia wapiganaji katika kwenda kudhibiti mambo, kinachoanzia kwanza ni elimu kwa wahusika na hatimaye kutakiwa wafuate taratibu na sheria.

Hata hivyo, katika eneo la uharibifu wa mazingira ieleweke kwamba wizara yangu imechukua hatua kadhaa za kuweza kudhibiti wahalifu hao wanaoharibu mazingira ya nchi yetu na kupora rasilimali zisizorejeshika za wakwezi na wakulima wa nchi hii, kuwadhibiti na kuwachukulia hatua. Tunaliomba Baraza la Wawakilishi pamoja na Wajumbe wake waendeleo kutupa mashirikiano pale tunapoamua kuchukua hatua na kuwadhibiti na kuwashurutisha sheria wale ambao hawataki kufuata utaratibu wa sheria bila ya shuruti. Ahsante sana. (*Makofi*)

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana, Mhe. Waziri nafikiri hakunielewa nilikuwa nikizungumza kwa haraka haraka labda nizungumze kidogo kidogo. Swali la pili nilipouliza nilisema *Mashaallah* amejaaliwa kuwa ni waziri mwenye vikosi na hii ni kazi ya sadaka na kule kumekuwa na uchimbaji wa mchanga kwa nini haweki ulinzi wa kutosha eneo lile la Mwanakwerekwe.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nafikiri unavunja utaratibu. Mhe. Salim.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi naitwa Simai sio Salim. Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunisahau.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi ningependa kumuuliza Mhe. Waziri pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa na kuyajibu yote. Kwa kuwa katiba zetu zote mbili ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar inatoa uhuru wa kuabudu na haki zote za kila Mtanzania na Wazanzibari zimetajwa katika katiba zetu zote mbili. Katika Wilaya yangu ya Kati kumekuwa na kilio cha wananchi wangu hasa waumini wa dini ya Kikristo kukosa eneo rasmi la kuzikiana miaka nenda miaka rudi, na tayari maombi yao yameshafika kwa Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa utekelezaji.

Je, Mhe. Waziri unanihakikishiaje kwa waumini hawa wenye kuamini dini ya Kikristo katika eneo la Wilaya ya Kati hasa katika jimbo langu la Tunguu katika maeneo ya Binguni, Mtakuja, Dunga, Mwera/Pongwe, Ubago, Jumbi na Tunguu yenyewe ili waweze kupata hii haki yao ya kuweza kuzika watu wao. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kabla hujajibu Wajumbe sauti inanifika huku na kama tunavyojua kuwa ukumbi wetu una *echo*, kwa hivyo, itakuwa hapati kujibiwa vizuri akasikia majibu yake naomba tuwe watulivu. Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Saleh Mohamed Said (Mpakabasi), Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Tunguu swali lake la nyongeza.

Utaratibu

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 37 lakini kianzio cha majibu ya Mhe. Waziri kataja jina ambalo sio langu kama ulivyotaja wewe mwanzo. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, Mheshimiwa mtaje jina lake vizuri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Simai (Mpakabasi). Mhe. Mwenyekiti, serikali imepokea maombi kama alivyosema yeye mwenyewe kupitia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Namuomba Mhe. Simai Mohamed aendeleo kufuatilia eneo lake ili taasisi zinazohusika za Halmashauri pamoja na Mkoa na Wilaya wakae pamoja wapendekeze eneo ambalo litakuwa muafaka katika kuwapatia mahitaji wananchi hao ambao hivi sasa mahitaji hayo hayapo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa sasa tunaendelea na utaratibu wetu kulingana na *Order Paper* ya leo ilivyo. Mhe. Jaku Hashim Ayoub uliza swali lako.

Nam. 180

**Mafunzo kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri namna ya
Kujibu Maswali Barazani**

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndio yenye dhamana katika chombo hiki cha wananchi katika kusimamia uwajibikaji wa Mawaziri na Naibu Mawaziri. Mhe. Rais wa Zanzibar katika kipindi kilichopita aliagiza Mawaziri kujibu kwa kina maswali wanayoulizwa na kama hawana jawabu wachukue muda watajibu kwa maandishi.

Je, ni lini Mawaziri na Manaibu Mawaziri watafanyiwa semina kuelekezwa namna ya kujibu maswali kama alivyoagiza Mhe. Rais, hasa kwa kuwa maswali yanayoulizwa yamezingatia maslahi ya Zanzibar na wananchi wake kutokana na umuhimu wake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 180 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliwaagiza Mawaziri kujibu kwa kina na umakini maswali yanayoulizwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili muulizaji na wananchi wanaoifuatilia vikao vya Baraza hili waridhike na majibu hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu jana katika majibu yangu ya msingi ya swali Nam. 144, kwamba bado tunaamini kuwa Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wanajibu vizuri maswali yao yanayoulizwa katika Baraza hili tukufu bila ya kuacha shaka yoyote, na inapotokea jibu linalohitaji takwimu au ufafanuzi wa ziada, waziri muhusika hutoa ahadi ya kujibu kwa maandishi na Waheshimiwa Mawaziri husika hutekeleza ahadi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi kuwa Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wanao UWELEDI mkubwa na wa kutosha wa kujibu maswali katika Baraza lako tukufu bila ya kuhitaji semina.

Hata hivyo, viongozi sote tunaelewa umuhimu wa semina na mafunzo yanayoweza kutolewa ndani na nje ya Baraza hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, nataka kumwambia Mhe. Waziri kuna msemo unasema kwamba: "*Huruma hailei mwana*", "*Mchelea mwana kulia mwisho hulia yeye*". Kwa kuwa siamini na hali halisi ya majibu tunayopata je, yuko tayari kukamata Mas-hafu na kuzungumza hayo anayoeleza ambayo bado yanatia shaka na hali halisi, Mas-hafu ambao ninao hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa uliza swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ninachouliza yuko tayari kukamata Mas-hafu yeye mwenyewe amekuwa akifanya mazoezi ya kukaa na kuinuka kuwalinda mawaziri, juzi hapa tumeshuhudia, yuko tayari kukamata Mas-hafu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hilo katika swali mama halimo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa siamini na hali halisi ya majibu tunayopata je, yuko tayari kukamata Mas-hafu na kuyazungumza hayo anayoeleza ambayo yanatoka ndani ya moyo wake. Hilo la kwanza bado la pili Mheshimiwa.

Kwa kuwa semina lengo lake ni kuwajengea uwezo Mawaziri na Manaibu Mawaziri hasa ambao hushika nafasi hizo kwa mara ya kwanza, je, ni lini mafunzo haya yatatolewa kwa Mawaziri na Manaibu Waziri wapya.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri jibu swali la pili.

Mhe Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, tunapotoa kauli zetu mbele ya Baraza lako tukufu huwa hatutoi kwa kula viapo vya Mas-hafu, tunafanya hivyo tukiamini kwamba chombo hiki ni kikubwa na sisi kwa upande wa mawaziri tunatekeleza wajibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nirudie tena kwamba Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wanafanya wajibu wao wa kujibu maswali, wanaelewa

taratibu zote. Ikumbukwe kwamba serikali inawajibika kwa pamoja, pale inapotokea kwa yeyote yule binadamu kughafilika basi serikali inachukua nafasi hiyo kutoa ufafanuzi wa ziada ama kujibu swali kama lilivyo. Kwa hivyo, bado naamini majibu yanajibiwa kwa ufasaha na kwa utaratibu ulivyo. *(Makofi)*

Kuhusu swali la pili la mafunzo, kama nilivyosema hapa si Mawaziri, si Manaibu Mawaziri, si Wajumbe wa Baraza hili siku zote kujifunza ni jambo la msingi, kwa hivyo, hakuna anayekataa kujifunza na elimu haina mwisho, na ndio maana kunakuwa na semina za mara kwa mara hapa ndani na wakati wowote ikiwepo semina nyengine itafanyika. Lakini mawaziri hawa wanajua utaratibu wa kujibu swali bila ya kuwafanyia semina. Kila waziri anakuja kwa wakati hapa anafuata utaratibu anapoitwa na Mhe. Spika na Naibu Spika ama Mwenyekiti wanafuata utaratibu huo na wanajibu maswali na hakuna siku ambayo Baraza limekaa bila ya kujibiwa swali, kwa msingi huo maswali yanajibiwa kwa ufasaha na yanakidhi haja. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, mimi ningeomba kuuliza swali la ziada kwa Mhe. Waziri. Kwa kuwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri mara nyingi wanapokuja kutujibu maswali baadhi ya siku hujibu maswali ambayo sio ya ripoti hasa nyengine kama zina udanganyifu lakini sio kupitia wao ni kupitia watendaji wao. Je, mawaziri kupitia wizara zao watawachukulia hatua gani wale watendaji wanaowapa ripoti za uongo na wanapokuja kutujibu maswali yetu yanakuwa sio ya kweli.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni utaratibu linapoulizwa swali lazima watendaji na wataalamu wa wizara walipitie na kulifanyia kazi ili watoe majibu yasio shaka, yatakayoridhisha Wajumbe na ni wajibu wa mawaziri kuliangalia na pale ambapo wanaona lina kasoro inatakiwa walirekebishe ili majibu yakitoka hapa yatoke kwa umakini. Ni haki ya kila waziri anapoona kuna mtendaji mzembe atekeleze wajibu wake kuchukua hatua zinazofaa ili kusiwe na uzembe na mambo yote yaende kama yalivyopangwa. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa pamoja na majibu tunayopewa na Mawaziri pamoja na Manaibu Mawaziri wengi wao ukiwauliza wanakwambia watakujibu kwa maandishi. Je, haoni kama ni udhaifu huu kwa mawaziri hao. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, moja katika utaratibu wa kujibu maswali kujibu kwa maandishi ni haki ya waziri muhusika. Hivyo basi, maswali hujibiwa kwa ukamilifu wake kwenye swali la nyongeza kama litakuwa na takwimu au linahitaji maelezo ya ziada ambapo kwa wakati huo waziri hana majibu sahihi, anayo haki ya kujibu kwa maandishi.

Nam. 6

Haki ya Ajira kwa Watu wenye Ulemavu

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Aliuliza:

Kwa kuwa Sura ya 3 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 12(1) kinasema kuwa "Watu wote ni sawa mbele ya Sheria, na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa...". Na kwa kuwa miongoni mwa haki za msingi za binadamu ni kufanya kazi na kupata ujira ambayo imeelezwa katika kifungu cha 21(3).

Kutokana na maelezo ya vifungu hivyo vya Katiba, serikali imejipanga vipi kuona kuwa Watu Wenye Ulemavu wenye sifa wanafaidika na haki zao hizo za Kikatiba.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984 imelinda haki za msingi za binadamu ikiwemo usawa mbele ya sheria na haki ya kufanya kazi.

Katika kuhakikisha kwamba hakuna mtu atakayebaguliwa katika fursa za ajira, Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 kifungu cha 58 kifungu (2) na kifungu 59 kifungu (1) imeweka vigezo vya kupata fursa za ajira katika utumishi wa umma ikiwemo kiwango cha elimu na sifa kulingana na nafasi ya kazi inayohitajika. Kwa msingi huo watu wenye ulemavu nao pia wanayo

fursa ya kupata ajira ilimradi wanazo sifa zinazolingana na nafasi ya kazi iliyopo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa uwezo wa Serikali wa kuwaajiri vijana wakiwemo wenye ulemavu kwa sasa ni mdogo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kwamba vijana wakiwemo wenye ulemavu wananufaika na haki zao za Kikatiba za kufanya kazi. Miongoni mwa hatua zinazochukuliwa na serikali ni pamoja na kuwashajihisha vijana kujiunga na vikundi vya ushirika vya hiyari ili waweze kupatiwa mikopo serikalini na kuweza kujiajiri, ambapo serikali kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imetoa jumla ya mikopo 337 (Unguja 261 na Pemba 76) yenye thamani ya Tshs. 523,428,000/= kwa mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mpango wa kuwajengea uwezo vijana wakiwemo wenye ulemavu walioamua kujihusisha na ujasiriamali kwa kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali na hatimaye kuwapatia mikopo ili waweze kujiajiri wenyewe. Mpango huu kwa sasa unatekelezwa na Wizara inayoshughulikia masuala ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwa vijana wote wakiwemo wenye ulemavu kujitokeza ili kuzitumia fursa za ajira zinapotokezea. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa inasemekana kuwa watu wengi wenye ulemavu huwa wanakosa kuajiriwa kutokana na hali zao.

(a) Serikali ina mikakati gani ili kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wenye sifa wanapatiwa ajira.

(b) Katika maelezo yake alieleza kuwa kuna watu wenye ulemavu ambao wamepatiwa fursa za mikopo kwa ajili ya kujiendeleza na ujasiriamali. Je. Mhe. Naibu Waziri anieleze ni watu wenye ulemavu au vijana wangapi wameweza kupatiwa fursa hizo na wao wakaweza kujiajiri.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, serikali imekuwa ikijitahidi

katika suala la kuwaajiri wanapoajiri wanaajiri watu mbali mbali wakiwemo watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kusoma kifungu namba 30 cha Kanuni ya Utumishi 2014.

"Itakapotokezea watu wa makundi maalumu wana sifa sawa na watu wengine katika masharti ya ajira kipaumbele cha ajira kitatolewa kwa watu wa makundi maalumu".

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kanuni yetu ya utumishi inavyoelezea hivyo hivyo ndivyo tunavyofanya. Iwapo pale watatokezea watu, watatokezea vijana wenye sifa moja ambayo kuna kazi moja, na kuna vijana wawili mwenye ulemavu na aliyekuwa hana ulemavu, kwa hiyo kama wale watakuwa na sifa moja basi kipaumbele kitatolewa kwa wale watu wenye ulemavu. Hivyo ndivyo ilivyo, ndivyo ambavyo tunafanya na vile vile si watu wenye ulemavu tu, vile vile panapotokeza ajira pakiwa pana wanawake na wanaume kwa hivyo mara nyingi huwa tunawapa wanawake kipaumbele zaidi kuliko wale wanaume.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, si siri kwamba dunia nzima inajulikana hasa nchi za kifaraka watu wenye ulemavu walikosa sifa za kuweza kupata fursa za kuajiriwa kutokana na changamoto kadhaa zinazowakabili wenyewe watu wenye ulemavu pamoja na nchi zao, serikali kidogo hatusemi walibezwa lakini nchi zilikuwa zina changamoto, fursa walikosa za kuweza kupata sifa za kuweza kuajiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, nchi nyingi duniani zimeweka mkakati na sheria maalumu ambazo zinawapelekea watu wenye ulemavu kuweza kuajiriwa. Mkakati na sheria maalumu inawapelekea watu wenye ulemavu waweze kuajiriwa kutokana na kukosa sifa.

Je, wizara yake ina mkakati gani kuweka sheria maalumu za kuweza kuajiri ili kuwapa kipaumbele watu wenye ulemavu kwa sababu walikosa sifa huko tulikotokea.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ni kwamba sheria ya watu wenye ulemavu pamoja na mambo mengine inaelezea suala zima la namna gani ya kupatiwa ajira serikalini na sehemu nyenginezo. Kwa maana hiyo, sheria ambayo tunayo sasa hivi ambayo inasimama kwa watu wenye

ulemavu nahisi kwamba inatosheleza. Lakini wazo lako tutalichukua na pale ambapo tutahisi kwamba upo umuhimu wa kufanya hivyo bila shaka tutafanya hivyo.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni sehemu ya dunia na sasa hivi dunia inakabiliwa na tatizo la ajira ikiwemo Zanzibar yenyewe. Wakati wowote inapotokezea nafasi ya kazi kwa mujibu wa sheria ya Utumishi serikali inatoa tangazo la wanaotaka ajira, na kwa bahati nzuri tunakuwa na waombaji wa ajira wengi sana kuliko nafasi zenyewe. Lakini kwa utaratibu uliokuwepo baadae kunakuwa na *short list* ya wale ambao wanachaguliwa kufanya usaili na mambo mengine. Sasa zipo tuhuma kwamba wale wanaokuwepo katika *short list* baadae unapofanyika uteuzi.

(a) Kwenye usaili baadhi ya watu wanapewa majibu kabla ya usaili wenyewe na kufanya usaili huo.

(b) Hakuna matokeo yanayotangazwa baada ya usaili huo, na waliochaguliwa badala yake watu wanapigiwa simu kienyeji na kuambiwa wewe tayari uende kazini na wale waliokosa hawaarifiwi kama wamekosa na wamekosa kwa sababu gani na kiwango gani kilisababisha ukose.

Je, serikali kupitia Wizara hii ya Utawala Bora ina mpango wowote wa kutoa haki kwa waomba kazi wote kuzijua sababu gani zilizosababisha wakakosa, na kwa sababu gani mwengine akapata, kutakuwa na *list* ambayo itabandikwa na kuonekana wazi wazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, serikali bado hatujapata taarifa ya hizo tuhuma kama kuna baadhi ya masuala ya usaili yanayotayarishwa na taasisi husika kwamba yanapenya kwa hao wahusika ambayo wanafanyia usaili. Lakini kama lipo hilo tunaomba tuweze kushirikiana na tupe taarifa ili tuweze kuwachukulia hatua ipasavyo hawa wanaofanya vitendo hivyo visivyokubalika katika serikali yetu hii. Ahsante. (*Makofi*)

Nam. 66

Kuwekwa ATM Mashine eneo la Baraza la Wawakilishi

Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Aliuliza:

Kwa kuwa Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) imekuwa na wateja wengi wanaotumia Benki hiyo wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na

watumishi wa Baraza. Na kwa kuwa huduma ya kutumia mashine ya *ATM* inarahisisha sana, huduma za Benki na haitumii muda mwingi.

Je, Wizara yako ina mpango gani kuanzisha huduma hii katika eneo la Baraza la Wawakilishi, Chukwani na lini itaanzishwa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 66 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi kuwa *ATM* zinasaidia sana na kurahisisha huduma zinazotolewa na Benki, kwa kuelewa hili Beki ya Watu wa Zanzibar imedhamiria kuongeza idadi ya *ATM* zake na kuziweka katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

Hivi karibuni tayari *PBZ* imenunua *ATM* mashine 15 ambazo zinatarajiwa kufungwa katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

Moja ya *ATM* hiyo itafungwa katika eneo la Baraza la Wawakilishi hapa Chukwani. Kazi za ujenzi wa kibanda zinaendelea na uwekaji wa *ATM* hiyo utakamilika ndani ya mwezi wa Oktoba mwaka huu. (*Makofi*)

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa pongezi za dhiti kwa serikali na Wizara ya Fedha kwa kuamua kuchukua juhudi binafsi, na kwa kuwa hii ilikuwa ni ahadi ya muda mrefu tangu Waziri wa Fedha aliyepita kwamba sasa mumeamua kuweka mashine ya *ATM* katika eneo la Baraza la Wawakilishi.

Kwa kuwa jitihada mbali mbali zimekuwa zikifanyika za kuwapunguzia usumbufu wananchi wetu pale wanapokwenda kutaka huduma katika mabanki yetu. Lakini bado huduma zimekuwa hazikidhi haja hasa ifikapo tarehe za mwisho wa mwezi. Je, ni upi sasa mkakati wa serikali katika kuhakikisha pindipo unapofika katika siku zile wananchi wetu wanakuwa wanakosa usumbufu ule na kuwapunguzia adha katika mahitaji wanayoyataka.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwa kupunguza msongamano ambao Mhe. Mihayo Juma N'hunga ameuona katika benki zetu ndio maana benki kwa makusudi kabisa inadhamiria kuongeza idadi ya *ATM* katika maeneo mbali mbali, na katika kipindi cha hivi sasa ndani ya mwaka huu *ATM* zitawekwa katika Vituo vya Kibweni KMKM, Mpirani tutakuwa na

mashine 4 eneo la Mpirani kwenye Makao Makuu ya Benki ya Kiislamu. Lakini Kivunge itakuwepo, Chwaka itakuwepo, Paje tunakusudia kuweka, Mahakama Kuu itakuwepo, Malindi, Kinyasini, Mahonda, Vitongoji, Konde na Micheweni.

Kwa hiyo, hizi zinazofungwa na zilizopo tutakuwa na idadi karibu mashine 32, na utaratibu wa kuziongeza kadri hali ya kibiashara itakavyoimarika katika maeneo mbali mbali hadi mashine hizi zitawekwa, na tunalielewa kwamba katika vipindi vya mwisho wa mwezi kutokana na mahitaji makubwa ya mishahara watu kuchukua mishahara yao Benki huwa inaweka utaratibu maalumu wa ku-*restock* fedha katika mashine zile ukiacha siku za kawaida.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa kuwa huduma ya *VISA* ni muhimu hasa ukizingatia kwamba nchi yetu inapokea wageni ambao wengine ni watalii na wengine ni wafanyabiashara, ili waweze kupata huduma ya *VISA* katika mahitaji mbali mbali kwa kupitia hizi mashine za *ATM* pamoja na mabanki yetu. Ni lini huduma hii ya *VISA* itaweza kurudishwa katika kisiwa cha Pemba hasa baada ya Benki ya *Barclays* kufunga tawi lake Pemba.

Pili, katika maeneo mengi ambayo hizi *ATM's* zinafungwa, watu wenye ulemavu hasa wale wenye ulemavu wa kutumia vigari wanakosa nafasi ambazo tunasema ni *wheel chair bound access*, ukiangalia na haziendi na *standard* za kimataifa hasa kwa mujibu wa sheria za walemavu na mahitaji yao yaliyokuwepo. Ni utaratibu gani utahakikisha katika maeneo ambayo zitafungwa hizi mashine mpya ambazo nimezitaja ili kuhakikisha walemavu wa aina zote waweze kupata hizo huduma katika maeneo husika. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie kwamba mashine zote hizi zitakuwa ni *ENV Compact* kwa maana zitachukua *master* na *VISA Cards*. Hizi mpya na hizo zilizokuwepo nazo zote zimerekebishwa *system* yake ili kuweza kutumika kwa *VISA* na *Master Cards*.

Hili la pili la kufanya mashine hizi ziwe *accessible* kwa watu wenye ulemavu. Hili tunalichukua ni wazo zuri, jema, tutawasiliana na wataalamu kuona kwamba mashine hizi zinakuwa *accessible* kwa makundi mbali mbali ya kijamii.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kuniona.

Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri na ya ufasaha naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa sababu Benki ya Zanzibar (*PBZ*) imejenga umaarufu mkubwa sana nje na ndani ya Zanzibar kwa kutumia mtandao wake wa *WorldRemit Day* na kwa sasa mtandao huo haufanyi kazi ipasavyo.

Je, ni sababu gani za msingi ambazo tunakosa huduma hizo mara kwa mara.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba arudie taratibu swali lake.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa rudia swali lako Mhe. Waziri alielewe.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Benki yetu ya Zanzibar (*PBZ*) imejenga umaarufu mkubwa sana nje na ndani ya Zanzibar kwa huduma yake ya *WorldRemit*, na kwa sababu hiyo mtandao huo umekuwa ukikosekana mara kwa mara kwa hivi sasa.

Je, ni sababu gani za msingi ambazo tunaweza kukoseshwa huduma hiyo muhimu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, sikuli- *capture* lile neno naomba alirudie hilo neno mtandao gani.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): *WorldRemit Western Union.*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, nikiri kwamba ndio nasikia sasa hivi kuwa huduma hii imekosekana. Sasa naomba kwa sababu sitaki kulidanganya Baraza lako, naomba Mhe. Mwakilishi anikubalie kwamba nitampa majibu kwa maandishi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan...! Samahani Mhe. Hassan kaa kitako wameshatimia wawili, Katibu.

Nam. 22

Usambazaji wa Huduma ya Umeme Vijijini

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia Kanuni ya 39(4) swali langu hili ninaliondosha, na sababu ya kuliondosha swali hili utekelezaji wake tayari umeshafanyika. Ninawashukuru sana Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kuniletea umeme Pangatupu.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

(Swali hili limeondoshwa na Mhe. Mwakilishi aliyetaka kuliuliza)

Nam. 175

Ukomesaji wa Shughuli za Ukataji Minazi

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): - Aliuliza:

Hali ya ukataji wa minazi katika kisiwa cha Unguja ni mbaya sana, pamoja na jitihada zinazofanywa na Wizara kupitia Idara husika.

Kwa kuwa minazi inakatwa, na kupelekwa katika viwanda mbali mbali Unguja. Je, Mhe. Waziri ni hatua gani madhubuti zilizoandaliwa juu ya kukomesha tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali naomba kutoa maelezo mafupi kidogo kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sensa ya Miti ya mwaka 2013 (*Zanzibar Wood Biomass Survey*, 2013), visiwa vya Unguja na Pemba vina minazi inayokisiwa 3,332,421 (Unguja 2,288,042 na Pemba 1,044,379). Tathmini hiyo imebaini kwamba Unguja ipo minazi mikongwe 261,529 na Pemba 111,882 isiyozaa kabisa.

Mhe. Spika, tunakiri kwamba suala la kuhifadhi rasilimali ya minazi ni jambo muhimu sana ili kuendelea kupata mazao ya nazi kwa ajili ya mahitaji yetu ya chakula na ziada kusafirisha nje ya nchi ili kupata fedha za kigeni. Hata hivyo inabidi tukubali kuwa minazi ikifikia umri wa miaka 60 na kuendelea huwa

inakatisha uzazi na hapo inabidi kubadilisha matumizi yake. Minazi yenye umri kama huo ni mizuri kwa kutoa mbao za kujengea na fanicha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana utamaduni wa kutumia mbao za mnazi kwa ajili ya ujenzi na fanicha hapa kwetu umeanza hivi karibuni katika miaka ya 1990. Kabla ya hapo visiwa hivi havikushuhudia matumizi makubwa ya mbao za minazi. Kazi ambayo ilihusisha matumizi ya magogo ya minazi ilikuwa ni uchomaji wa chokaa. Kazi hii ilihusisha zaidi minazi mipevu ambayo imekufa au ile iliyokuwa haizai kabisa. Hivi sasa utaratibu huo haufuatwi na minazi inakatwa bila ya kujali kama ni michanga au mipevu, yenye kuzaa na isiyozaa.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa ukataji miti hapa nchini unatakiwa kufanywa kwa mujibu wa Sheria, lakini wahalifu wengi wamekuwa wakikata miti hiyo bila ya kufuata Sheria. Utaratibu uliopo ni kuwa muhusika anatakiwa awasilishe maombi yake kwa kujaza fomu ambayo inapitia kwa Sheha wake, Wilayani na hatimaye Idara ya Misitu ambayo ndio inayotoa kibali cha ukataji kwa mujibu wa Sheria.

Mhe. Mwenyekiti, hatua zinazochukuliwa na Wizara katika kukabiliana na tatizo la ukataji wa minazi ni pamoja na:-

- (a) Kusimamia utekelezaji wa Kanuni ya Kudhibiti Matumizi ya Misumeno ya moto kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa lengo la kupunguza uharibifu;
- (b) Kufuata utaratibu wa Sheria wakati wa ukataji miti na kukaguliwa miti ambayo imeombwa kukatwa, sambamba na kuhamasisha upandaji wa miti;
- (c) Kutoa elimu kwa wakulima, masheha, pamoja na kutumia vyombo vya habari vya Redio na TV kuhusu umuhimu wa kuihifadhi minazi na kuendelea kupanda mipya.
- (d) Kutayarisha programu maalumu ambayo itasimamia masuala yote yanayohusu minazi *“Zanzibar Coconut Development Program”*.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, historia ya Zanzibar ilikuwa ni sehemu mojawapo inayozalisha nazi nyingi na kuweza kuuza Tanzania Bara, na Mwenyezi Mungu

alivyotujaalia katika nchi yetu kwa upande wa Kisiwa cha Pemba zao kubwa ni karafuu. Kwa Unguja kama ilivyosemwa kwenye takwimu ni minazi. Lakini hii minazi kwa upande mwingine inakatwa upande wa Unguja tu ukiacha upande wa Pemba kidogo inanipa mashaka. Si kuna mpango maalumu wa kuhujumu uchumi wa minazi hapa Unguja.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwakilishi hakuna kitu kama hicho, lakini niweze kusema labda Pemba ni wasikivu zaidi kuliko Unguja. (*Makofi*)

Katika misumeno ambayo tumeikamata labda niseme Pemba ni misumeno 40 kwa mwaka huu na kwa Unguja ni misumeno 25. Kwa hivyo, Pemba hawawahi kufikia kuikata ile minazi tunawahi kuwakamata na misumeno yao. (*Makofi*)

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na mimi naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, ni mbegu gani ya minazi ambayo wizara imefanyia utafiti na kuwaelekeza wakulima kuweza kuitumia.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hamida Abdalla Issa swali lake kama ifuatavyo.

Mbegu ambayo imeshauriwa kuoteshwa ni *East African Tall* ni ile minazi mirefu, vile vile kuna minazi inaitwa *Malay dwarf* nayo pia hiyo pia imeshauriwa kuoteshwa ambayo inakubaliana na hali ya hewa ya nchi yetu.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nishukuru kwa majibu ambayo tunapata kutoka kwa Mhe. Naibu Waziri na mimi naomba niulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b)

- a) Kwa kuwa Mhe. Waziri kakiri na kusema zipo aina mbili za minazi ambazo zinafaa kupandwa katika maeneo hasa kwenye Kisiwa chetu cha Unguja. Lakini ukitazama katika eneo letu la Kizimbani pale ipo minazi ambayo imepandwa inafika miaka kumi lakini mpaka sasa haitoi mazao kama vile ambavyo Wizara imekusudia.

Je, upi sasa ama lipi sasa ilikuwa lengo la Serikali kuweza kupanda minazi ile.

- b) Kwa kuwa Serikali imekuwa na *double standards* katika kuzuia ukataji wa minazi katika Kisiwa chetu cha Unguja. Kuwakataza Wazanzibari wanyonge ambao wengine hukata minazi yao iliyozeeka na kuruhusu mwekezaji anayekata minazi kwa kutumia mashine eti kwa kuwa ni Mzungu. Je, hivi sasa kauli ya Serikali kuhusiana na Mzungu huyu anayeendelea kuimaliza, kuiteketeza na kuathiri zao zima la minazi katika Kisiwa chetu cha Unguja.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:
Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

- a) Kwanza pale Kizimbani ni kweli tumeotesha minazi hiyo ambayo ni miaka kumi sasa hivi haina mazao. Pale panaitwa ni kituo cha utafiti, siyo kila unachokifanya kwamba unafanikiwa, kuna vitu unafanikiwa na kuna vitu hufanikiwi. Ndiyo maana hatukuwapa wananchi wapande mbegu hiyo na ndiyo maana nikasema ninayoshauri ni *East African Tall* na *Malay Dwarf*. Mbegu hiyo tumeachana nayo kabisa.
- b) Kuhusu kauli ya Serikali Mzungu huyu anaruhusiwa kwa sababu anakata vibali na minazi inayoruhusiwa ni ile ambayo imeshafika miaka 60 ndiyo inayokatwa, na haikatwi minazi ambayo ipo chini ya miaka hiyo.

Nam. 143

Kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi ya Walimu

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza :-

Kwa kuwa uanzishwaji wa Tume ya Utumishi ya walimu ni miongoni mwa Mapendekezo ya mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNESCO na ILO yanayozitaka nchi wanachama kuhakikisha zinaunda Tume hizo katika nchi zao.

- (a) Je, Wizara haioni kwamba ipo haja ya kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi ya Walimu

- (b) Je, Sera ya elimu ya Zanzibar ya mwaka 2006 inasema nini kuhusu suala la walimu kuwa na chombo hicho cha kusimamia ajira ya walimu hao.
- (c) Je, Wizara imefanya mchakato gani wa kuandaa mapendekezo ya kuundwa Tume hiyo hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Namba 143 lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:- Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa kuwa Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *UNESCO* na *ILO* yalipendekeza kwa nchi wanachama wa mashirika hayo kufikiria kuanzishwa kwa vyombo vya kupanga maslahi ya walimu na kulinda miiko na maadili ya taaluma hiyo. Hilo lilikuwa pendekezo ambalo nchi wanachama wa umoja huo kutekeleza kulingana na mazingira ya nchi zao.

Katika hali hiyo, uanzishwaji wa chombo au vyombo vya kupanga maslahi na kulinda maslahi ya walimu umetofautiana baina ya nchi moja na nyengine kutokana na mazingira ya nchi hizo. Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

- a) Wizara imelipokea wazo la kuanzishwa kwa chombo kitakachosimamia ajira, sifa, miiko na maadili na maslahi ya walimu na inaendelea kulifanyia kazi. Wakati muafaka utakapofika, Wizara itachukua hatua kulingana na mazingira ya nchini kwetu.
- b) Sera ya Elimu ya Zanzibar mwaka 2006 katika sura ya 6 ukarasa 41 imetamka maneno yafuatayo ya Kiingereza “*There shall be a single authority for recruitment of teachers*” maana yake kwa lugha ya Kiswahili “kutaanzishwa Mamlaka moja itakayosimamia uajiri wa walimu” pamoja na Sera ya Elimu kutoa tamko hilo, utekelezaji wa Sera yenyewe unafanyika hatua kwa hatua na haimaanishi kuwa masuala yote yaliyotajwa katika sera yatatekelezwa mara moja.
- c) Wazo la kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu, limekuwa likizungumzwa katika vikao mbali mbali na hivi karibuni katika warsha ya kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu wa Zanzibar, Mwaka 2016 hadi

2020 suala hili limejitokeza. Mchango wa mawazo unaotolewa katika vikao unapokelewa na napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi mawazo hayo yanafanyiwa kazi na hatimaye uamuzi muafaka utatolewa na Wizara kwa kushirikiana na vyombo vinavyohusika vya Serikali.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri lakini kwa kuwa Chama cha Walimu huwa kinashauri Serikali na Serikali yetu ilivyo sikivu huwa inapokea huo ushauri na kuufanyia kazi. Kwa hivyo, naomba kujua Mhe. Mwenyekiti, je, jambo hili litachukua muda gani na hata kuundwa kwa Tume hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Nassor Salim Ali kama ifuatavyo.

Tumeleza wazi kwamba suala hili ni la mchakato, yaani linahusisha mazungumzo ya wadau mbali mbali inahusisha taasisi nyengine za Serikali lakini pia inahusisha kujifunza uzoefu wa mataifa mengine na nchi nyengine katika suala la kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu.

Hivi sasa kwa mfano tumekuwa tukifunza katika nchi za Afrika. Nchi ambazo labda zimefanikiwa katika kuanzisha taasisi hizi na zile ambazo hazijaanza. Kwa hivyo tumekuwa tunajifunza na katika eneo letu nchi ambayo pengine imepiga hatua kidogo ni nchi ya Kenya. Lakini napo pia tumeona kuna matatizo ambayo yamezuka.

Sasa kuanzisha taasisi ambayo itafanya kazi kama tulivyokusudia, tunahitaji kufanya utafiti wa kina. Pia tunahitaji mazungumzo na wadau mbali mbali hasa taasisi nyengine za Serikali, kwa sababu hili ni suala la kisheria pia. Kwa hivyo, mchakato huo utakapomalizika wakati wowote Tume hii itaanzishwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kama sikosei ninajua kunako maskuli yetu Zanzibar tuna upungufu mkubwa wa walimu, pia kama sikosei kila mwaka Zanzibar na Tanzania kwa jumla

inazalisha walimu wengi wenye digrii na diploma ambao wapo mitaani hawana ajira.

Na walimu hawa huwa wanaajiriwa Tanzania Bara hasa wenye digrii, siku hizi wamekuwa wanaajiriwa Bara kwa sababu Zanzibar kutokana na kuwa hawaajiriwi. Je, Wizara yake ina mkakati gani maalumu wa kuajiri vijana wetu hawa ambao wapo mitaani na wana elimu tayari na maskulini kwetu hakuna walimu na vijana wapo, kwa kuwaajiri hawa ambao tayari wameshasoma na wanaajirika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hassan Khamis ambaye ni Mwakilishi wangu kama ifuatavyo.

Ni kweli kwamba kila mwaka tunatoa wahitimu ambao wamesomea katika masuala ya walimu. Ni kweli kwamba baadhi ya vijana wanaajiriwa katika taasisi za elimu Tanzania Bara, lakini ukweli kwamba wapo ambao mpaka sasa hawajapata ajira. Kwa hivyo Serikali itaendelea kuajiri pale ambapo kibali cha uajiri kitakopatikana kutoka Serikalini.

Kwa mfano katika mwaka huu wa fedha tumeomba au tumekisia kuajiri wafanyakazi zaidi ya mia tisa katika Wizara ya Elimu wakiwemo walimu. Lakini na hivi karibuni tu Serikali imetangaza nafasi za ajira za walimu wa sayansi ambao hawapungui sabini na mchakato huo unaendelea na utakapokamilika wakati wowote wataajiriwa walimu hao. (*Makofi*)

Nam. 148

Tatizo la Kurusha Matangazo ZBC

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

ZBC ni chombo cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kinachotoa habari za ukweli na uhakika, lakini inaonekana haina nguvu ya kurusha matangazo kwa Zanzibar na Tanzania yote kwa jumla.

- a) Je, Serikali ni lini italiiondoa tatizo hilo.
- b) Je, Serikali imejipangaje, kuwasomesha na kuwaongezea uzoefu na ufanisi watangazaji wake na kuimarisha miundombinu ya mitambo yake.

c) Kwa nini waandishi wa *ZBC* hasa katika kisiwa cha Pemba hawaonekani kutafuta habari na kuingia katika ushindani na waandishi wengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 148 lenye kifungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kwa sasa *ZBC* mitambo yake ya kurushia matangazo ina matatizo. Hivyo basi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo inachukua hatua mbali mbali za kutatua matatizo ya urushaji wa matangazo katika vyombo vyake vya *ZBC TV* na *ZBC Redio*.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua mitambo ya vituo hivyo ni ya gharama kubwa, lakini tayari imeshaagiza mitambo ambayo itawezesha kuongeza nguvu ya matangazo ya *ZBC* yaweze kufika mbali na kuwa na ubora.

b) Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Shirika la Utangazaji, linachukua hatua kadhaa za kuwasomesha wafanyakazi wake katika fani mbali mbali kwa mafunzo ya ndani na nje kwa lengo la kuwaongezea ujuzi wa utaalamu watendaji wake. Katika kipindi cha 2015/2016 jumla ya wafanyakazi 40 wamepata mafunzo nchini China, Misri, Zambia pamoja na Tanzania Bara, kwa kada za habari, utayarishaji vipindi, ufundi, utangazaji na utawala. Wafanyakazi wengine bado wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika vyuo mbalimbali nchini na nje ya nchi.

Aidha, Shirika la Habari la Ujerumani *DW* limeendelea kuwapatia mafunzo kwa kuwaleta wataalamu wake, kwa lengo la kuwapatia ujuzi na utaalamu wafanyakazi wa *ZBC*. Jumla ya kozi 6 zimefanyika katika kipindi cha mwaka 2015/2016.

c) Mhe. Mwenyekiti, napenda nilieleze Baraza lako tukufu kwamba waandishi wa habari wa *ZBC* Pemba, wanashiriki kikamilifu katika kutafuta habari, na kukabiliana na ushindani kama waandishi wengine kwa sasa kwa wastani hurusha habari moja mpaka tatu kwa siku. Pia hushiriki katika ziara za viongozi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, lakini mimi kidogo pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, nataka nimuulize tena

Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza, kutokana na umuhimu mkubwa wa chombo chetu hiki cha ZBC. Kwa sababu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kauli zake na maelekezo yake yote yanaitupia ZBC kutangaza ili wananchi wake kupata matangazo ya ukweli na uhakika. Hili Shirika mwanzo lilikuwa ni idara, baadae tukaona tulipe nguvu liwe shirika ili kukuza mitambo yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli bado haijawardhisha kabisa wananchi wake kupata matangazo kwa kupitia ZBC kwa Zanzibar nzima haijaweza kujikimu. Inawezekana hata TV ambazo zinatoka Bara basi tunapata matangazo zaidi kuliko hii. Sasa nilikuwa namuuliza Mhe. Naibu Waziri.

(a) Je, anafhamu umuhimu wa malengo, madhumuni na umuhimu wa kuanzishwa kwa chombo hiki cha TVZ.

(b) Je, serikali haioni umuhimu wa kutafuta mbinu mbadala ili kuwapatia wananchi matangazo bora, matangazo kwa urahisi, matangazo bila malipo ili wananchi wapate habari kutokana na chombo hiki cha serikali yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, serikali inafhamu kwamba kutafuta mbinu mbadala ya kuboresha haya matangazo yetu au kupata matangazo vizuri kwa wananchi wake wa Zanzibar. Namwambia Mhe. Mwakilishi kwamba serikali inajua hilo na ndio maana sasa hivi, nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba serikali imo katika kuagizia mitambo mipya kwa ajili ya kukiboresha chombo hiki na wananchi wake wapate matangazo.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa misingi ambayo imewekwa na wazee wetu pamoja na Hayati Marehemu Mzee Karume, kwa kutumia vyombo hivi vya habari kutoa elimu, kuwaelimisha wananchi wetu Wazanzibari wote umuhimu wa mambo tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni tumeanza kuona kwamba viongozi wetu wa dini wakitoa kauli tofauti hasa katika uzazi wa mpango, pamoja na serikali ambayo inachokizungumza. Sasa Mhe. Naibu Waziri unatwambia leo Wazanzibari wakamate kauli ipi. Uzazi wa mpango au waendeleo kuamini na kuwasikiliza viongozi wa dini kwamba hii ni neema na Mwenyezi Mungu ametuletea. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kujibu swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo. Mhe.

Mwenyekiti, ni kweli vyombo vyetu vya habari nia na dhamira kubwa ni kutoa elimu kwa wananchi wetu na tunafanya hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli serikali inaelimisha juu ya kuchukua mpango bora wa uzazi, lakini Masheikh wana wajibu wao kwa masuala ya dini na sisi sote ni waumini wa dini, hivyo huwezi kuwakataza Masheikh walisilime linalozungumzwa na dini zao. Kwa hivyo, Masheikh na viongozi wengine wa dini wanayo haki ya kuyazungumza kinachozungumza kitabu, na ndio wajibu wa viongozi wa dini. Wajibu wa serikali ni kuona yale ya kilimwengu tunayoyaona tuweze kuwaeleza wananchi wetu ili kuepuka athari zake.

Vile vile serikali inawaambia wananchi na kuheshimu dini zao na inapenda sana wananchi wafuate taratibu za dini na wakati huo huo wasikilize maelezo ya serikali kwa nia ya kuepusha athari ambayo inaweza kutokea. Sasa uzazi wa mpango ambao serikali inauhumbiri na kueleza ni jambo la msingi na tungewaomba wananchi wafuate. Lakini hatuwakatazi wananchi kusikiliza mawaidha yanayotolewa na viongozi wao wa dini. *(Makofi)*

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Je, ni kwa nini wafanyakazi wa ZBC kutoka Pemba hatuwaoni kuja kuchukua taarifa au kuchukua habari katika Baraza letu la Wawakilishi linapoendelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naungana na Mhe. Mwakilishi kusema kwamba ni kweli wafanyakazi wetu kutoka Pemba hawashiriki katika kutoa matangazo kwenye Baraza hili tukufu unapofikia muda wake. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Mwakilishi kwamba suala hili nalichukua na nitalifanyia kazi na hatima yake atawaona wafanyakazi wetu kutoka Pemba na wao wanashiriki katika Baraza hili kupata matangazo. Ahsante.

Nam. 58

Upatikanaji wa Huduma za Afya Katika Jimbo la Birikau

Mhe. Suleiman Makame Ali - Aliuliza:-

Kwa kuwa suala la Afya ni jambo la msingi kwa kila binaadamu. Kwa kuwa bila ya kuwepo huduma za afya zilizo bora maisha ya binaadamu yatakuwa hatarini. Kwa kuwa kumekuwepo na jitihada za kujenga vituo vya afya ili kuwafikishia wananchi huduma hizo, katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu. Je, ni kwa nini mpaka hivi sasa kituo cha Afya Birikau hakijamaliza kujengwa

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia kuwa na afya njema na wazima katika kutimiza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar ambao wametuleta katika ukumbi huu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi maarufu Sheikh wa Ndagoni, swali lake nambari 58 kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa afya ni jambo la msingi kwa kila mwananchi, na ndio maana imetamkwa kwa ufasaha kabisa katika *manifesto* ya wakati huo ya *Afro Shirazi Party* ya mwaka 1967, na Zanzibar ni miongoni mwa nchi chache sana duniani ambayo ina sera ya kutoa huduma za afya kwa wananchi wake bila malipo. Miongoni mwa nchi zinazotoa huduma za afya ulimwenguni bila ya malipo ni kama ifuatavyo.

Nchi zenyewe ni:

1. Denmark
2. Norway
3. Qatar
4. Sweden
5. UAE na
6. Zanzibar yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, ukilinganisha nchi zote hizo zina wastani wa pato la zaidi ya dola 10,000 kwa mwananchi tofauti na vile ilivyokuwa Zanzibar ambayo iko chini ya dola 1,000 kwa mwananchi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi sasa Zanzibar imeshapata cheti pia cha uthibitisho cha kufikia malengo ya milenia ya kuwa na vituo vya afya chini ya kilomita 5. Sisi tuko katika wastani wa kilomita 3.5. Lengo kuu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuendelea kuwafikishia wananchi wake huduma hizo kadiri ya hali ya fedha itakavyoruhusu.

Katika mantiki hiyo hiyo naomba nimjibu pia Mhe. Mwakilishi kuwa Kituo cha Afya Birikau kitamalizwa pale tu tutakapokuwa tumekamilisha taratibu za kifedha na hilo litashughulikiwa mara moja. Ahsante (*Makofi*)

Mhe. Suleimna Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Nina imani ya kwamba ulizungumza kuwa kila kwenye kilomita 5 ni kwa kupitia ilani hii ya CCM mnayoitekeleza, wananchi wangu wa Shehia ya Ndagoni Jimbo langu hilo hilo la Ziwani wao wenyewe wamejenga Kituo chao cha Afya kwa kupitia wafadhili.

Je, ni lini serikali kwa kupitia wizara yako utawakamilishia kituo kile kwa kuwatilia vifaa na madaktari, ili kuanza kazi na kuweza kuwapunguzia wananchi adha inayowakabili kwa kufuata masafa marefu huduma hiyo ya afya.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mhe. Suleimani kwa swali lake la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali kwamba fedha zitakapopatikana basi katika bajeti zetu hizi na hicho kituo kitashughulikiwa. Lakini wakati huo huo kuna vituo kama 9 Pemba ambavyo vyengine kuna nguvu za wananchi ambavyo wameanza wao wenyewe kujenga havijakamilika, kuna vituo vyengine vilipata athari ya kupasuka ambavyo vinahitaji ukarabati wa kina sana, kuna vituo vyengine vilichomwa moto navyo pia inabidi vifanyiwe marekebisho.

Kwa hivyo, kwa upande wa wafanyakazi katika kituo hicho cha Mhe. Mjumbe alichokitaja, basi hilo nitalifuatilia kwa haraka sana, ili tuweze kuwapeleka hao wafanyakazi na kituo kiweze kufanya kazi yake ya kutoa huduma kwa jamii moja kwa moja.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na mimi kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Waziri, katika majibu yako umetwambia kwamba kwa Pemba kuna vituo 9 ambavyo vitaendelea kurekebishwa na kutengenezwa ili viweze kufanya kazi. Je, vipi kuhusu Unguja. Kama na Unguja vipo vituo hivi, je unatwambia nini kuhusu Kituo cha Mbuzini.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Hidaya Ali kwa swali lake la nyongeza, nilikuwa natarajia atakitaja Kituo cha Mbuzini.

Mhe. Mwenyekiti, katika orodha ya wafadhili ambao tunafanyanao kazi pamoja, vituo vyote katika orodha hizi za pamoja ORIO, MILELE na SMZ bajeti yake moja kwa moja, kwa Unguja ni vituo 17. Lakini Mbuzini naomba

nimwambie Mhe. Mjumbe kuwa kile ni kituo maalumu, kwa sababu kile kina ahadi ya Mhe. Rais moja kwa moja, ya kukipandisha hadhi na daraja kufikia ngazi ya Wilaya. Kama jana alivyouliza Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) wa Jimbo la Mpendae, kile kina mpango maalumu. Huo mpango sasa hivi unaendelea kupangwa na Mhe. Rais naye analifuatilia kwa karibu, kwa sababu ni ahadi yake ya moja kwa moja. Mara tu tutakapokamilisha hii miradi yetu mikubwa, basi nguvu zetu zote na mimi mwenyewe nitahamia Mbuzini kwa hili. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afya, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Mhe. Waziri kakiri kwamba Kituo cha Afya cha Mbuzini ambacho kinatarajiwa na wananchi wa Magharibi "A" kuwa hospitali yao ya Wilaya, ina ahadi ya Mhe. Rais, na kwa kuwa Wizara ya Afya inaendelea kufanya utaratibu wa kumalizia ujenzi wake.

Je, kwa kipindi hiki Mhe. Waziri haoni kwamba kuna haja kwa Hospitali ya KMKM Kibweni, ambayo juzi juzi tu imewaajiri madaktari bingwa 7, kutamka kuwa ni Hospitali ya Wilaya ili kuwanusuru wananchi wa Wilaya ya Magharibi "A" ambao ndio kimbilio lao kwa sasa.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, vituo vyote vilivyokuwa chini ya vikosi, KMKM, pamoja na kile cha Bububu JWTZ na vituo vyengine vyote vinavyotoa huduma kupitia vikosi. Vituo hivi vina utaratibu maalumu na sheria zao maalumu.

Jambo ambalo tunashirikiana nao pamoja na Wizara ya Afya, ni kwa kuwa wao mbali ya kuwatibu wale askari wa vikosi vyao, basi hizo huduma huziongeza na kutanua zaidi kufikia kwa wananchi moja kwa moja. Sisi kwa upande wetu wa Wizara ya Afya huwa tunashirikiana nao kwa karibu sana, kwa sababu tunajua wanasaidia kutoa huduma zile kwa jamii moja kwa moja, kwa hivyo wao tunashirikiana zaidi. Lakini utaratibu wao uko bado kwenye masuala yao ya kijeshi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo tunaendelea kufanya hivi sasa tunashirikiana nao kwa upande wa madaktari, huwa tunapata madaktari kutoka kwao wanakuja kwetu wanatibu, kwa sababu kuna madaktari wenye taaluma maalumu kutoka kwetu wanakwenda kwao. Pale tunapopata mgao wa madawa pia huwa kadiri uwezo unavyoruhusu tunawapatia na wao dawa. Lakini kutoa tamko moja kwa moja kwamba kituo hicho sasa kiwe ndio kituo kikuu, mamlaka yale hayapo katika Wizara ya Afya. Kwa hivyo, hatuwezi kutoa

tamko hilo, mamlaka hayo yapo katika wizara husika ambayo inashughulikia KMKM. Lakini naomba hivyo vituo viendelee kubakia kwa sababu vinafanya kazi vizuri sana na vinaendelea kutoa huduma nzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwapongeze pia Waheshimiwa Wawakilishi ambao huwa wanatoa mchango mkubwa sana kwa baadhi ya vituo vya vikosi ambavyo viko katika majimbo yao, pamoja na *ambulance* ambayo niliikabidhi hivi karibuni mimi mwenyewe. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa leo hili ndio swali letu la mwisho la Wizara ya Afya.

Waheshimiwa Wajumbe, katika ukumbi wetu huu leo wa Baraza la Wawakilishi kuna wageni ambao wametufikia hapa kwa leo siku ya Tarehe 30/09/2016.

Wageni wenyewe ni Jumuiya ya Vijana ya Kupambana na Udhalilishaji Mkoa wa Kaskazini Unguja maarufu unaitwa (UVKUKA) ukiongozwa na Mkuu wa wa Msafara huo ni ndugu Hafidh Mohammed Juma na msaidizi wake ndugu Haji Shehe Haji, tunaomba wasimame tuwatambue (*Makofi*)

Nasema ahsanteni sana karibuni katika ukumbi wetu musikilize mijadala inavyoendelea na naomba tuwatambue uwepo wao Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hapo tunaendelea.

MAOMBI (PETITION)

Maombi ya Wananchi Kuhusu Kuchukuliwa Hatua za Haraka za Kuepusha Usumbufu Usiokuwa wa Lazima kwa Kupatikana kwa Huduma Mbali Mbali za Afya Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kabla sijaweka hoja yangu naomba uniruhusu kwa dakika mbili tu kwa heshima na taadhima, kabla sijatoa maelezo haya nina maombi haya kwa niaba ya wananchi kusema kwa dakika tatu.

Kwanza nimpongeze kwa dhiti, kutoka ndani ya sakafu ya moyo wangu Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa mafanikio ya afya si haba yamepatikana ikiwemo *ICU* imetengenezwa, Huduma za wazazi zimeimarishwa, upatikanaji wa dawa umepewa kipaumbele katika *quarter* hii

ya bajeti, upanuzi wa hospitali ya Mnazi Mmoja, Jengo la mama na Watoto unaendelea, Hospitali ya Mnazi Mmoja inaelekea kujitegemea.

Nampongeza pia kwa kusimamia ilani na kwa kutekeleza kwa vitendo ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015/2020 hususan katika kuimarisha sekta ya afya nampongeza sana Mhe. Rais.

Pili Mhe. Mwenyekiti, kama Mwakilishi ninayefahamu majukumu yangu ya kazi katika chombo hichi kwa mujibu wa kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar cha mwaka 1984, kwa kufanya wajibu huu sio nia yangu kuikomoa Serikali ya Chama changu cha Mapinduzi, au mtu yeyote, nimekuwa mstari wa mbele kusimamia sekta ya afya tokea nilipokuwa Mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii katika Baraza la Nane na baadhi ya watu wakasema nilikuwa namkomoa aliyekuwa Naibu Waziri wakati ule, lakini sasa hivi hayupo na bado naendeleza kutekeleza wajibu huo.

Katika Baraza la Nane mkutano wa 17 kikao cha 4 cha Tarehe 17/10/2014 nilileta hoja binafsi ya kuitaka Serikali kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha huduma za afya kwa wananchi, lakini hadi leo hii Serikali haijaleta majibu, ya kipi wametekeleza, kipi bado na wana mkakati gani wa kutekeleza mapendekezo hayo, wanaoathirika ni wananchi wapiga kura wetu. Kwa kutambua hilo wamenituma na kunipa maombi hayo kuomba basi angalau zile huduma muhimu za Hospitali za Mnazi Mmoja zipatikane. Hivyo lengo langu ni kumsaidia Mhe. Rais kufuatilia watu aliowapa kazi na kutekeleza ilani ya chama kwenye sekta ya afya, sote humu ndani tulimuahidi Mhe. Rais wakati akizindua Baraza la Tisa mnamo tarehe 5/04/2016 kuwa tutaifanyia kazi hotuba ile kwa vitendo, kwa kufanya hivyo hatutomuogopa wala kumuonea mtu haya, nami ndio natekeleza ahadi ile katika eneo hili la afya na mengineyo kwa vitendo, si dhambi Mwakilishi kufanya wajibu wake kikatiba.

Baada ya kueleza hayo kwa kifupi sana naomba kuwasilisha maombi haya ya wananchi kama ifuatavyo Mheshimiwa Mwenyekiti.

Maombi ya Wananchi Mhe. Mwenyekiti, nafikiri itakuwa jambo la kwanza katika Baraza lako hili kutokea, sikumbuki kama kuna *reference* kama hii imeshawahi kutokea.

Maombi ya Wananchi Kuhusu Kuchukuliwa Hatua za Haraka za Kuepusha Usumbufu Usiokuwa wa Lazima wa Kupatikana kwa Huduma Mbali Mbali za Afya Katika Taasisi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar

(Maombi haya yamefanywa na Mheshimiwa JAKU HASHIM AYOUB, Mwakilishi wa Wananchi jimbo la Paje, kwa niaba ya Wananchi ambao orodha ya majina na saini zao imeambatanishwa pamoja na maombi haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 27 (1) (f) na (n) na Kanuni ya 30 (1) mpaka (6) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2012)

MADAI YA MSINGI YA OMBI

Kwa mujibu wa Kanuni ya 30 (3) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2012, wananchi ambao majina na saini zao yameambatanishwa sambamba na ombi hili wana madai ya msingi ya kufanya ombi hili, ambayo nayawasilisha kwa niaba yao mbele ya Baraza hili kama ifuatavyo:-

1. Taasisi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja haina sehemu rafiki ya huduma za wateja/wananchi. Msingi wa dai hili ni kwamba wananchi wanapofika Hospitalini hapo kupata huduma wanakumbana na matatizo ambayo hawana sehemu ya haraka ya kuyasemea, kwa vile hakuna kitengo au pahala maalumu na rafiki pa kupatiwa ufumbuzi au maelezo, kwa mfano wananchi wanafika hawapatiwi taarifa kuwa huduma fulani haipatikani badala yake wanatumia muda mrefu kusubiri, wapo baadhi yao wanatoka maeneo ya nje ya mji kuanzia asubuhi mpaka mchana hawapati huduma na hawaelezwi kwa nini hazipatikani.
2. Kumekuwa na Usumbufu wa Kupatikana baadhi ya Huduma za Vipimo muhimu kwa Ukamilifu wake. Msingi wa dai hili ni kuwa baadhi ya wananchi waliofata huduma za “*Ultra Sound*” wamekuwa wakifika mapema asubuhi Hospitali na kukuta tayari kuna idadi maalumu ya watu wasiozidi 20, imeshawekwa kufanyiwa kipimo hicho na wengine kutakiwa kurudi hadi siku ya pili.

Wananchi wengine wamedai kuwa kipimo muhimu kama “*x-ray*” kimekuwa na usumbufu kwa wagonjwa wanaofika hapo mapema asubuhi hadi mchana hawajapata huduma hiyo, aidha kipimo hicho hakifanyiki kwa baadhi ya maeneo ya mwili kama vile mgongo, tumbo, kiuno na maeneo ya kichwa badala yake kinafanyika kwa maeneo ya mkono na miguu. Baadhi ya wagonjwa wameambiwa kuwa mashine kubwa ya ‘*x-ray*’ imeharibika muda mrefu na iliyopo ni ya ‘*mobile*’ ambayo kifaa chake cha kusoma filamu chache zilizopo (*automatic processor*)

inaharibika mara kwa mara wakati mwengine huduma hiyo husita kutolewa.

3. Baadhi ya Miundombinu muhimu ya Hospitali haiipo katika hali nzuri ya kuridhisha na kuwapa wasiwasi wananchi wa kupatikana huduma kwa wakati na bila kusita. Msingi wa dai hili ni kuwa baadhi ya maeneo yenye vifaa muhimu vya tiba kama ‘*C.T Scan*’ paa lake linavujiwa na limezibwa kwa ‘maboksi’ hali inayoviweka hatarini vifaa vya mashine hiyo. Wananchi wanadai kuwa eneo la Upasuaji (*theatre*) na Chumba cha Uangalizi wa Karibu (*ICU*) vinakosa umeme, wakati umeme unapozimwa ule wa dharura wa jenereta haufiki maeneo hayo muhimu kwa maisha ya mtu. Wananchi hao wamepata hofu kuwa hali inakuwaje kama tatizo hilo linatokea wakati mgonjwa anahudumiwa sehemu hizo? Wananchi hawa pia wanadai kufahamu kuwa kumekuwa na uchelewaji wa kupatikana kwa “*Oxygen*” inayopatikana ni kwa ajili ya dharura tu. Wananchi hawa wanalalamika kuwa eneo kama la Upasuaji linaonekana limechoka likiwa na *furniture* duni, milango na madirisha yakiwa yamechakaa.
4. Baadhi ya Watoa Huduma kuonekana wanazidiwa na kazi ama kutokana na uchache wao au kuondoka maeneo yao kabla au baada ya wakati kwisha. Wananchi hawa wanadai kuwa baadhi ya maeneo wanaotoa huduma huwa wachache au mmoja tu na idadi ya wanaosubiri kupatiwa huduma ni kubwa, na kusababishwa mgonjwa anapofika asubuhi kuondoka mchana pengine hiyo huduma awe hajaipata, mfano eneo la ‘*x-ray*’ ambalo wapo watu nne tu wanaongia kwa zamu na mara nyingi wakati wa kutoa huduma huwapo mtu mmoja tu, aidha wanadai kuwa chumba cha huduma za ‘*x-ray*’ hakina vipoza hewa (*A/C*).
5. Baadhi ya Huduma za Mama Wajawazito zinahitaji kuimarishwa zaidi. Msingi wa madai haya ni wananchi kwanza kupongeza hatua za kuondoa ada ya mama wajawazito kujifungulia, hivi sasa hawalipishwi, hata hivyo wamepata wasiwasi juhudi hizo huenda zikarudishwa nyuma na kutopatikana kwa baadhi ya vifaa vya kujifungulia au vinavyopatikana kuwa chini ya kiwango, mfano wananchi wamedai kuwa jiki zinazopatikana hivi sasa zipo chini ya kiwango hazina hata harufu na hata “*urinary bag*” hazipatikani.

MADHUMUNI YA OMBI

Kutokana na madai hayo ya wananchi, madhumuni ya kuleta ombi hili mbele ya Baraza la Wawakilishi ni kuitaka Serikali hii tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambayo ni sikivu na yenye kujali shida za wananchi:-

1. Kuweka haraka kitengo cha huduma za wananchi ambacho kitafanya kazi muda wote kuwasaidia wananchi kupata maelezo ya matatizo mbali mbali wanayokumbana nayo wanapofika Hospitalini hapo kupata Huduma.

Aidha mpango wa kuvaa beji maalumu zenye majina kwa wafanyakazi wa Hospitali uanze mara moja ili wananchi wajue watu wanaowahudumia na endapo litatokea jambo lolote waweze kuwatambua.

2. Mpango maalumu wa kuimarisha huduma za vipimo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ufanyike kwa kuimarisha vifaa tiba, kuvifanyia matengenezo mara kwa mara bila kungojea viharibike kwanza ili viweze kuendelea kutoa huduma bila kusita na pawepo mpango unaofahamika kwa wananchi kupatiwa huduma bila kusongamana na kusubiri muda mrefu wakati wanafika mapema.
3. Kurekebisha miundombinu ya Hospitali kama vile kuhakikisha umeme wa dharura unapatikana 'ICU' na chumba cha upasuaji, endapo umeme wa kawaida utakapozimwa. Aidha jenereta lililoharibika muda mrefu lifanyiwe marekebisho kwani liliopo limeazimwa kutoka Hospitali ya 'Mental' nalo pia linatumika kwenye ujenzi. Vile vile maeneo yanayovuja yafanyiwe matengenezo ili vifaa visiharibiwe na maji, vumbi na mwanga wa jua na maneneo yenye ubovu kama eneo la wagonjwa wa kisukari sakafu yake imeharibika, na kwa niaba ya waleta maombi haya nitatoa mifuko mitano ya saruji kuchangia matengenezo yake.
4. Huduma za mama wajawazito zihakikishwe zinatolewa kwa viwango kwani zipo kesi za uzembe zinajitokeza ambazo huenda huko siku za mbele zikaigharimu Serikali.

SABABU ZA KUSOMWA OMBI

Kwa kuwa juhudi mbali mbali zinafanyika kuimarisha huduma za afya za wananchi, na kwa kuwa wananchi hao wana imani kubwa na Serikali yao katika kuimarisha huduma za afya kupitia juhudi hizo; ni muhimu

kusomwa ombi hili la wananchi la kutaka hatua za haraka zichukuliwe kuondoa usumbufu wa upatikanaji wa huduma katika Hospitali.

Aidha, Kamati Maalumu ya wajumbe watatu iundwe kufuatilia kila hatua na kila mara utekelezaji wa ombi la wananchi la kushughulikia madai ya wananchi hao na taarifa iwasilishwe Barazani au kwenye Kamati husika ya Kisekta, kwa vile madai haya yanatokana na changamoto ambazo wananchi wetu wanakumbana nazo kila siku na hawana pahala pa kusemea Serikali ikasikia kwa haraka sana isipokuwa katika chombo hiki kitukufu cha Baraza la Wawakilishi.

Kwa niaba ya Wafanya maombi naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe ombi limeletwa mbele yetu, sasa niwahoji wale wanaokubali wanyooshe mikono, wanaokataa. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Afya: Kama alivyosema Mheshimiwa muwasilishaji namshukuru hii ni mara ya kwanza kuwasilishwa ombi kama hili, na nilikuwa najaribu kupitia kanuni hapa hususan kifungu cha 30 kuanzia moja mpaka 6 sasa ningeomba muongozo wake Mhe. Mwenyekiti, na kupitia kwa wataalamu wetu makatibu uliokuwa nao kwamba ombi hili wangetuelekeza linahojiwa ndani ya Baraza ama halihojiwi la kwanza. Maana hiyo kunyoosha mkono ni kama tunapiga kura ya aina fulani, la kwanza hilo.

Lakini la pili naomba muongozo wako katika upande wa Serikali, kwa sababu Mheshimiwa wakati anawasilisha maombi yake ameigusa Serikali moja kwa moja, na baadhi ya huduma hizi zinatolewa na serikali inatimiza majukumu yake kwa wananchi wake, na Serikali pia inasimamia watumishi hao wa umma ambao wanatoa huduma hizi kwa wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri endelea kama ulikuwa hujamaliza.

Mhe. Waziri wa Afya: Kwa hivyo katika la pili nilikuwa naomba muongozo wake, kwa sababu Mhe. Mjumbe kwa kutumia haki yake nampongeza sana ametumia haki yake ya kuwasilisha maombi ya wananchi, na Serikali pia ina jukumu lake kwa sababu ameigusa Serikali moja kwa moja katika huduma ambayo ni nyeti sana, ambayo Serikali inatoa kwa wananchi wake, na pale sisi Wizara ya Afya tuna wafanyakazi

takriban elfu nne katika Wizara nzima ambao wanahudumia wananchi moja kwa moja, kwa hivyo kwa ripoti hii wameguswa.

Kwa hivyo nilikuwa naomba kupata muongozo wako, je, na pia kama itawezekana pia kupata muongozo wa Mwanasheria Mkuu kwamba Serikali inatoa majibu yake vipi, tunatoa leo leo, sisi tuko tayari, lakini tunatoa leo leo ama muongozo gani utakaofuata baadae. Kwa sababu hilo halijaelewa moja kwa moja kwenye Kanuni nimejaribu kutafuta halimo moja kwa moja kwenye kanuni, kwa hivyo naomba muongozo wako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Hapa katika ombi hili linaweza likapelekwa kwenye Kamati na baadae taarifa ikaletwa kwenye kamati, lakini pia Serikali ipo naonyalishia kwa hivyo inaweza ikatoa kauli.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ombi limewasilishwa na kanuni yetu inaeleza vizuri kanuni ya 30(4) inasema baada ya kutimiza masharti ya fasili ya tatu ya kanuni hii Mjumbe muwasilishaji wa ombi hilo atataja kwa ufupi sababu za kutaka ombi hilo lisomwe au kwamba liwasilishwe mezani, au lipelekwe kwenye Kamati teule au ombi linalohusika lichapishwe. Lakini hakutakuwepo na mjadala wowote kuhusu ombi la namna hiyo.

Msingi wake hapa nilivyomfahamu Mheshimiwa aliyewasilisha anataka lifike Serikalini lifanyiwe kazi, kama kuna mapungufu yarekebisha na kwa utaratibu wetu wa kiserikali mengi aliyoyasema yamo katika utaratibu wa kufanyiwa kazi ili kupata majibu sahihi. Nia na dhamira ya Serikali hii ni kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora za afya na huduma nyengine muhimu.

Kwa hivyo napenda kulipokea ombi aliloleta na Serikali itazidi kufanyia kazi pale ambapo itaona yapo mapungufu ili kurekebisha mapungufu hayo.

Nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali imeweka kipaumbele sana katika kutoa huduma za afya na kama alivyosema yeye mwanzo hapa hatua mbali mbali zimechukuliwa, kwa hivyo na hizi ambazo amezionesha zipo zinazoendelea kuchukuliwa, na kwa vyovyote vile kila ambapo pana kasoro kasoro hiyo itarekebisha ili huduma ziwe bora.

Mhe. Mwenyekiti, nataka aelewe kwamba katika dunia ya leo hata nchi kubwa duniani zinatoa huduma za afya kwa malipo makubwa, lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa imani ya wananchi wake inatoa huduma hizo bila ya malipo, na wananchi huchangia tu pale ambapo wanatakiwa kufanya hivyo kutokana na hali yetu ya kiuchumi, na hivi sasa jitihada zaidi zinafanywa ili wananchi wasichangie hata kidogo ili Serikali itoe huduma hizo kwa asilimia mia moja.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri amelitolea ufafanuzi kauli Serikali imeipokea, kwa hivyo tunaendelea.

HOJA YA MJUMBE

Hoja ya Mjumbe Kuhusu Ukiukwaji wa Sheria kwa Baadhi ya Taasisi Ambazo Zinatakiwa kuwasilisha Taarifa zake mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa Mujibu wa Sheria

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu sana, Mola wa viumbe wote.

Vile vile nikushukuru wewe kwa kukubali kuisoma hoja yangu hii leo mbele ya Baraza lako tukufu chombo hichi kikubwa cha wananchi.

Naomba nichukue fursa hii kuishukuru sana Serikali chini ya Makamo wa Pili wa Rais naye kukubali kusoma hoja yangu hii ikiwa na dhamira kubwa ya kuikumbusha Serikali juu ya mambo mbali mbali ambayo yanaweza kutokea ama ya kuweza kukiuka sheria hizi za Mashirika na Taasisi za Umma.

Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Mpendae kwa kuendelea kuniamini na kuweza kuni-*support* kila ninapofanya kazi zangu kisheria na kikatiba ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, hoja hii nimeitayarisha chini ya Kanuni ya 27(1)(n) pamoja na Kanuni ya 27(3) na Kanuni ya 49(1) Kanuni ya 50 ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012.

Maelezo ya Hoja

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kuwa Baraza la Wawakilishi limepitisha sheria zilizoanzisha Taasisi mbali mbali za Serikali ambazo sheria hizo zilitakiwa kuletwa ndani ya Baraza la Wawakilishi, ripoti ya mwaka kuhusu Taasisi hizo, na kwa kuwa kumekuwa na ukiukwaji wa sheria na baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma ambazo zilitakiwa kuwasilisha taarifa zake mbele ya Baraza kwa mujibu wa sheria na baadhi ya Taasisi hizo hazijawasilisha au hazijaletwa katika Baraza hili pale zinapotakiwa uwasilishaji wake haukidhi masharti ya sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa kutowasilisha kwa taarifa hizo mbele ya Baraza lako ni ukiukwaji wa sheria za nchi na kulikosesha Baraza taarifa muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa Taasisi hizo zilizoainishwa hapa nchini zina umuhimu mkubwa katika maendeleo ya nchi, na hivyo ni muhimu taarifa hizi zikawasilishwa katika chombo cha uwakilishi wa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi hizo ambazo zilitakiwa kuwasilisha taarifa zake mbele ya Baraza lako Tukufu pamoja na sheria inazozitaka Taasisi hizo kuwasilisha taarifa hizi mbele ya Baraza hili ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuzitaja Taasisi hizo:

Taasisi ya Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar kwa kifupi *ZIPA*.
Mhe. Mwenyekiti, Sheria Namba 4 ya mwaka 2002 katika kifungu chake cha 27 kinamtaka Waziri anayehusika na masuala ya fedha kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu mara tu baada ya kupokea ripoti ya mwaka kuhusu taarifa ya Mashirika ya Umma kwa mwaka uliopo na mafanikio yake katika miaka 2 ijayo. Taarifa ya mwaka ya fedha na taarifa ya ukaguzi wa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, uzoefu unaonesha kuwa taarifa kuhusu Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar zimekuwa haziwasilishwi wakati wa mkutano wa bajeti ambapo taarifa hizo zinazungumzia kuhusu mapato na matumizi tu ya mamlaka, jambo hili ni ukiukwaji wa sheria, kwani taarifa hizo zinazotolewa hazikidhi masharti ya sheria husika.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Makadirio na Matumizi na Mapato na Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka

2016/2017 katika ukurasa 24 Waziri alielezea kuhusu mapato na matumizi ya mamlaka tu.

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi nyengine ni Taasisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yaani CAG.

Mhe. Mwenyekiti, unaweza ukashangaa ni kwa nini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu yeye mwenyewe hakaguliwi. Mhe. Mwenyekiti, nafasi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 112 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambapo pamoja na majukumu mengine iliyopewa Kikatiba pia analo jukumu la kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu namba 3 cha Sheria Namba 11 ya mwaka 2003. Pamoja na jukumu hilo Sheria ya Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2015, katika kifungu cha 36 kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na yeye akaguliwe kutoka miongoni mwa watu ambao watateuliwa na Mhe. Waziri anayehusika na masuala ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu 36 (4) kinamtaka Waziri anayehusika baada ya kukamilisha uchunguzi huo na kuwasilishwa kwake awasilishe ripoti hiyo mbele ya Baraza lako Tukufu ndani ya miezi 3 ya mkutano unaofuata wa Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili watakuwa ni mashahidi kuwa Baraza hili halijawahi hata mara moja kupokea taarifa ya ukaguzi unaoihusu Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali mbele ya Baraza lako Tukufu. Hata mimi nikiwa shahidi tangu niingie miaka 5 iliyopita huu wa 6 bado sijapata taarifa hiyo na sijawahi kuona ndio chanzo na umuhimu wa kuleta taarifa hizi kwako.

Mhe. Mwenyekiti, ya tatu ni Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA* ambacho tumepitisha sheria nyengine juzi tu ya kuweza kuunganisha na Taasisi nyengine. Sasa hapa hatari yake inakuja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Chuo hiki kimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 8 ya mwaka 1999 kama ilivyorekebisha na sheria ndogo ya kwanza namba 1 ya 2009, kifungu cha 50 cha sheria hii kinamtaka Waziri anayehusika na masuala ya elimu kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu vitu vifuatavyo:-

Vivuli vya taarifa ya mapato na matumizi pamoja na taarifa za mali na madeni ya Chuo kwa kila mwaka.

Vivuli vya ripoti ya ukaguzi na vivuli vya ripoti ya Makamo Mkuu wa Chuo.

Katika hotuba aliyowasilisha Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2016/2017 mbele ya Baraza lako Tukufu, taarifa hizi na vivuli vya ripoti ambavyo vilitajwa kwa mujibu wa sheria hazipo na wala vivuli vya taarifa hizo hazijawahi kuletwa. Kivuli cha ripoti ya Makamo Mkuu wa Chuo hakijawahi hata mara moja kuletwa mbele ya Baraza katika hotuba hiyo. Sehemu ambayo imeelezwa ni kuhusu Chuo cha Taifa cha Zanzibar *SUZA* ni ukurasa wa 13 ambacho kimeelezwa kuhusu huduma ya elimu, ushauri na utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, ya nne ni Shirika la Utangazaji *ZBC*. Shirika hili limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 7 ya mwaka 1997 ambalo katika kifungu cha 24 cha sheria hii, kimeeleza kuwa Waziri atawasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu taarifa ifuatayo:

Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Shirika na Taarifa za Mali na Madeni na Kivuli cha Ripoti ya Mkaguzi na Kivuli cha Ripoti ya Katibu Mtendaji wa Shirika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba ya Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kuhusu Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Fedha ya mwaka 2016/2017 kiambatanisho namba 1(a) ukurasa wa 44 kimeweka taarifa za mapato na matumizi ya Shirika, taarifa ya mali na madeni ya Shirika hilo na ripoti ya Katibu Mtendaji na Shirika havijawasilishwa. Ripoti ya Katibu Mtendaji ya Shirika haijawahi kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu hata mara moja tangu mimi niweze kuingia Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi nyengine ya tano ni Ofisi ya Mufti. Ofisi hii imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 9 ya 2001 ambapo kifungu cha 13(3) cha sheria hii kinamtaka waziri anayehusika ndani ya miezi sita baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi, taarifa ya mwaka itakayojumuisha:-

1. Mapato na Matumizi ya mwaka
2. Mali na Madeni
3. Ripoti ya Ukaguzi wa Fedha

Katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya mwaka 2016/17 ilieleza taarifa kwa baadhi ya Taasisi zilizojitengea lakini Ofisi ya Mufti haikuwemo isipokuwa katika ukurasa wa 47 katika kiambatanisho namba 1 kimefafanua kuhusu mapato na matumizi ya Ofisi hii tu. Hata hivyo sheria inataka taarifa ya Ofisi hii iwasilishwe ndani ya miezi 6 baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha ambapo kwa ratiba zetu za kikazi za Baraza taarifa hiyo itatakiwa kuwasilishwa katika mkutano wa Oktoba, ikijumuishwa na mambo yaliyotajwa kwa mujibu wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, nyengine ni Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar *ZURA*. Mamlaka hii imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 7 ya mwaka 2013 ambapo katika kifungu cha 27 cha sheria hii kinamtaka waziri anayehusika na masuala ya nishati kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, ripoti ya mwaka ya ukaguzi na ripoti ya mamlaka.

Mhe. Mwenyekiti, kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ya mwaka 2016/2017 ukurasa wa 38 na 39 hadi wa 40 waziri ameeleza kuhusu utekelezaji wa mambo iliyojipangia mamlaka na taarifa ya mapato na matumizi ya mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, tukirudi katika sheria ya taarifa hii haijajitosheleza kwani yapo baadhi ya mambo ambayo Wajumbe wa Baraza walipaswa kuyajua kwa mwaka mzima kuhusu mamlaka hii kile kilichowasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu ni sehemu katika ripoti ya mamlaka tu. Mamlaka hii imeanzishwa kwa mujibu wa sheria namba 4 ya mwaka 2006 ambapo katika kifungu chake cha 34 sheria hii kinamtaka waziri anayehusika kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu mambo yafuatayo:-

Ripoti ya mwaka, ripoti ya ukaguzi wa hesabu na ripoti ya mamlaka.

Katika hotuba ya bajeti ya Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ya mwaka 2016/17 ukurasa wa 24, 25, waziri ameeleza kuhusu mapato na utekelezaji wa malengo yake tu. Mara nyingi ripoti kuhusu Mamlaka ya Maji inayohusisha katika hotuba ya bajeti ya wizara husika ilizungumzia kuhusu mapato na matumizi tu, hivyo kuacha taarifa nyengine zinazotajwa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi nyengine ya 7 ni Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar *ZAECA*. Mamlaka hii imeanzishwa kwa mujibu Sheria Namba 1 ya mwaka 2012 ambapo katika kifungu cha 12 cha sheria hii

kinaeleza kuwa Mkugenzi Mkuu wa Mamlaka atatarisha ripoti ya mwaka, atawasilisha kwa Mhe. Waziri ndani ya miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka utakaojumuisha. Vitu hivyo vitakavyojumuishwa ni kama ifuatavyo:-

Ripoti ya Fedha ya Mamlaka.

Taarifa ya Shughuli zinazofanywa na Mamlaka na baada ya kupokea ripoti hizi itawasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu ambavyo havijawahi kuwasilishwa.

Mhe. Mwenyekiti, wakati waziri anayehusika na Mamlaka hii Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Akiwasilisha hotuba yake ya bajeti alieleza taarifa ya Mamlaka hii katika kitabu chake ukurasa wa 27, 28 na kwa kiasi fulani amekidhi masharti ya sheria. Lakini tunaomba sana taarifa kama hizi zikitajwa ziwe na maelezo na taarifa za kutosha ili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waweze kushauri vizuri Serikali, vile vile waziri ahakikishe kuwa taarifa iliyowasilishwa Baraza la Mapinduzi iwe ni taarifa hiyo hiyo itakayowasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, hizi ni baadhi ya Taasisi ambazo Baraza lilitakiwa kuwasilishiwa kwake taarifa hizi kwa mujibu wa sheria lakini taarifa hizi zimekuwa aidha uwasilishaji wake moja kwa moja au haziletwi na kukidhi sheria hizi.

Mhe. Mwenyekiti, kuwasilishwa kwa taarifa za ukaguzi au *Auditing report* na mawaziri wanaosimamia Taasisi husika ndani ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, uwasilishwaji wa Taarifa za Ukuguzi wa Hesabu mbele ya Baraza lako Tukufu kwa kawaida hufuata taratibu ule mawaziri wanaohusika na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuwasilisha mbele ya Baraza lako taarifa ya ukaguzi na baadae Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma (*PAC*) kuifanyia kazi taarifa hiyo na hatimaye Kamati huwasilisha ripoti yake mbele ya Baraza. Huu ni utaratibu wa kawaida, ambapo unafahamika katika mabunge mengi ya *CPA*, lakini kumekuwa na kujichanganya katika uwasilishaji wa taarifa hizi wakati sheria ziko wazi kabisa.

Kwa sababu mbali mbali taarifa ya ukaguzi ambazo zinawasilishwa na waziri anayehusika kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, lakini sheria zinatambua kuwa mawaziri wanaohusika na taasisi husika kuwasilisha

taarifa zao za ukaguzi mbele ya Baraza lako Tukufu jambo hili lisichanganywe na taarifa ambayo inafanyiwa kazi na Kamati ya PAC, kwani sheria zinazoelekeza jambo hilo zipo wazi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, sheria ambazo zinamtaka waziri anayehusika kuwasilisha taarifa zake za ukaguzi na fedha kuwa katika Mashirika au Taasisi zinazojitegemea. Ijapokuwa yapo baadhi ya Mashirika au Taasisi zilizoanzishwa kwa mujibu wa sheria kama hizo lakini hazitakiwi kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bandari ambalo limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 1 ya mwaka 2003, Shirika la Meli ambalo limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 3 ya mwaka 2013, Mamlaka ya Uwanja wa Ndege ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 8 ya mwaka 2011, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambao umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 2 ya mwaka 1998 na kufanyiwa marekebisho Sheria Namba 9 ya mwaka 2002 na kufanyiwa marekebisho tena Sheria Namba 9 ya mwaka 2005.

Mhe. Mwenyekiti, hapa niliitaja Bodi ya Mapato ya Zanzibar kuwa haiwajibiki kuletwa hapa lakini hili nataka niweke *hansard* sawa na kuweka hotuba yangu hii sawa kuwa Bodi hii ilitakiwa ilete lakini katika taarifa zake na Mhe. Waziri anayehusika na mambo ya fedha na alete uchunguzi wa hesabu zake na makusanyo yake kwa mwaka lakini hata hivyo haijawahi kuleta taarifa hiyo. Bodi nyengine ambayo ilitakiwa isilete ni Shirika la Biashara la Taifa ZSTC ambalo limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 11 ya 2011.

Shirika la Umeme ZECO ambalo limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 3 ya mwaka 2006. Mashirika na Taasisi zote nilizozitaja hapa juu zimeanzishwa kwa sheria, hata hivyo taarifa zake hazikutakiwa kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu na badala yake inaishia kwa mawaziri husika tu.

Hata hivyo tunaomba sana Serikali ijue na tuweze kubadilisha sheria hizi ili kuzileta Barazani na kuona kuwa uwakilishi huo wa wananchi unapata taarifa kwa mujibu wa sheria inavyokuja.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Taarifa

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba kidogo katika warka huu ili *hansard* isiende vibaya, tunataka kumarifu Mhe. Mjumbe kwamba Shirika la Bandari ambalo limeanzishwa kwa mujibu wa sheria ni namba 1 ya mwaka 2007 sio 2003. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mheshimiwa nimepokea.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, Kwanza awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha sote tukakutana hapa leo Ijumaa ni karibu na sala sasa.

Pia nachukua fursa hii kukupongeza na mimi kunipa nafasi na kwa kuzingatia muda uliopo na kwamba siku yenyewe leo ya Ijumaa Mheshimiwa nitachangia jambo japo kidogo kidogo kutokana na uzito wa suala lenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza najikita kwenye Shirika la Bandari. Shirika la Bandari kama tunavyofahamu kuwa ni jicho la uchumi wa nchi nyingi duniani ambazo hazina bandari. Lakini pia Mwenyezi Mungu katujaalia kwamba katika kisiwa chetu cha Zanzibar tuna bandari ya asili bandari ambayo lau kama tutakuwa tunaitumia vizuri au tunaendelea kuitumia mimi naamini kwamba bandari hii ingeweza kusaidia kwa asilimia pengine 50 ya bajeti ya Serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki nipoteze muda lakini napenda kuchangia kwa kusema kwamba Bandari ya Zanzibar pamoja na sheria zilizopo umefika wakati sasa tukaifanyia marekebisho taasisi zote ikiwa pamoja na bandari na viwanja vya ndege, naungana na mtoa hoja Mhe. Mohammed Said kwamba, ni lazima twende na wakati ulivyo. Pia, nataka tujiulize ikiwa sheria zimeelekeza hivi kwa nini baadhi ya taasisi za serikali zinashindwa kutekeleza wajibu wake.

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kushangaza na ni jambo la kusikitisha sipendi nilaumu viongozi wetu waliotangulia, lakini napenda kuishauri serikali kwamba sasa wakati umefika wa kufanya mabadiliko ya kisheria ili mashirika yote yaweze kuwajibika iwe ni lazima kwa mashirika yote na taasisi za serikali kuleta ripoti zake kwenye Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya ufanisi. Jambo hili naiomba serikali iache kigugumizi cha mambo haya, sisi lengo letu sote ni kuitumikia nchi hii, lakini inavyoonekana Mhe. Mwenyekiti, kwamba sheria iliyopo inatoa kinga kwa taasisi jambo ambalo sio vizuri, sasa umefika wakati

wa kufanya mabadiliko ya kanuni hizi na sheria za mashirika na taasisi za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, hebu tujiulize jamani sisi tuna bandari ya Zanzibar ni daraja la kwanza, tuna bandari ya Dar-es-Salaam kwa wenzetu wa Bara, wana bandari ya Tanga, lakini hebu twendeni tukaiangalie bandari ya Dar-es-Salaam ni kiasi gani bandari hiyo inatoa mchango wako kwa bajeti kuu ya serikali. Halafu turudi na kwetu sisi tufananishe na bandari yetu ya Zanzibar ni kiasi inatoa mchango kwenye bajeti kuu ya serikali, ni mchango wa kiasi gani. Lakini mimi naomba kwenye hili Waziri wa Fedha aje atuambie yatakapofika majumuisho kuna nini au ana wito gani juu ya taasisi hizi kuleta sheria zake au kuwasilisha hesabu zake Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini na ni imani yangu kwamba taasisi hizi zitakapoweza kubadilisha sheria zitaleta maslahi mawili kwa nchi hii. Kwanza zitaweka wazi mapato na matumizi wananchi wote ambao ni haki yao kufahamu basi watafahamu na wataweza kushauri njia gani itumike ili kukuza mapato yanayotokana na bandari. Lakini ikiwa sheria hizi zitaachwa kuwa hivi hivi bado tutaendelea kuwa Shirika la Bandari na Viwanja vya Ndege vitakuwa na makusanyo makubwa lakini mchango wake kwenye serikali utakuwa hauonekani kabisa, ama utakuwa ni mdogo au hauonekani kabisa. Kwa mfano, tukija kwenye Uwanja wa Ndege walisema wanakusanya karibu 1.2, lakini ukija kwenye matumizi zile pesa zote wanazirejea zinatumiwa. Hivyo, tujiulize kuna nini au ni faida gani ambayo tunaipata sisi, au sisi faida yetu ni kutajwa kama tuna Uwanja wa Ndege tu.

Mimi natoa wito kwamba wakati umefika wa kubadilishe, kwa hiyo, tubadilishe sheria, tubadilishe mambo mengi tunayoyaona yana maslahi ya nchi hii ili Wazanzibari waweze kufaidika na hili. Mhe. Mwenyekiti, njia pekee ni kuwasilisha ripoti zake kwenye Baraza la Wawakilishi hapa.

Mhe. Mwenyekiti, tukirudi tena kwenye upande wa bandari, leo tumeona bandari kuna watu pale wanafanya kazi zaidi ya miaka 15 hawajakuwa na mkataba wa ajira, yote hii inatokana na sheria walizonazo zinawaruhusu kufanya hivyo, na ripoti ingelikuwa inakuja hapa kwa ukamilifu tungeweza kuishauri ili tukatafuta namna gani njia bora ya kurekebisha sheria na tukawaomba watu wa Idara ya Utumishi wakashirikiana ili wale watu ambao wameshafanya kazi zaidi ya miaka 15 pale wakapata mkataba. Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kuona bandari yetu leo ya Zanzibar inashindwa na daraja la Kigamboni lililojengwa hivi karibuni la Magufuli, hivi tujiulize kulikoni?

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo mimi naunga mkono hoja ya Mhe. Mohammed Said, kuhusu mashirika haya...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tatu.

Mhe. Omar Seif Abeid: Jambo ambalo naunga mkono kuhusu hoja ya Mhe. Mohammed Said, kwa michango yake ni Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, hata kwenye dini Mitume walipewa amri ya kupeleka ujumbe lakini Mwenyezi Mungu anatwambia siku ya Kiama na yeye atawauliza hao waliopelekewa ujumbe jinsi walivyopeleka ule ujumbe kwa wale walengwa. Sasa inakuwaje yeye CAG anakagua wenzake, lakini yeye ripoti yake ya ukaguzi haifiki Barazani, hilo ni jambo la kushangaza. Kwa hiyo, mimi naomba marekebisho yafanyike kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu kwa nia njema kabisa. Mimi naamini sisi wajumbe tuliomo humu sote tuna nia nzuri kwa ajili ya serikali yetu. Serikali ni yetu lakini pia tukumbuke kwamba tuna wajibu kwa wananchi waliotuchagua kuwatumia, na tukumbuke pia siku ya mwisho Mwenyezi Mungu atakwenda kutuuliza tuliwatetea vipi hawa.

Kwa hiyo, ni wajibu tukumbuke kwamba kila binadamu ana makoksa na ana mapungufu, hakuna binadamu aliyekuwa yuko sawa, hata hiyo sheria tuliyoitunga hata tukirekebisha mara 50 bado itakuwa ina mapungufu kwa sababu tumeitunga sisi binadamu. Lakini ni wajibu wetu pale tunapona kwamba kuna jambo haliendi sawa na tuna uwezo wa kulitengeneza kwa ajili ya maslahi ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia kuhusu mamlaka ya maji. Mamlaka ya maji leo ZAWA tumeona kilio cha wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi wanaililia ZAWA matatizo yaliyopo na yote haya ni miongoni mwa mapungufu kama haya, lau kama ingelikuwa ripoti zake zinawasilishwa tena kwa wakati na wajumbe wakapata nafasi ya kuzichangia mimi naamini kwa asilimia kubwa tungeweza kuishauri na tatizo hili lingeweza kupatiwa ufumbuzi. Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya mimi nasema naunga mkono hoja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba tukumbuke kwamba muda wetu uliobakia ni mdogo, wachangiaji wameongezeka kuna mawaziri nao wanahitaji kutoa mchango wao. Kwa hivyo, watakaopata muda au tungoze muda, tutakubaliana lakini leo Ijumaa.

Wajumbe: Hapana!

Mhe. Mwenyekiti: Basi anayechangia aende kwenye *point* moja kwa moja ili tuokoe na Mhe. Waziri, aweze kutoa maelezo.

UTARATIBU

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, wakati wetu kama unavyoona na leo Ijumaa hautoshi, na wachangiaji waliokuwa wengi na wakati jioni tunakuja kufunga Baraza hili, tungeomba uweze kuwapa nafasi baada ya kurudi na hoja yenyewe hii ni muhimu sana ili wachangie kidogo na baadae basi itolewe hoja ya kufunga Baraza.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, nimekuelewa hivi kwamba tuvute muda wa jioni au tuendelee jioni unavyotaka wewe.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ninavyopendekeza siwezi kutaka kwenye kiti chako, lakini napendekeza kwenye kiti chako, wewe ndio muamuzi, jioni baada ya kuingia wachangiaji kama wapo wachangie kidogo na baadae basi tuweze kufanya kazi nyengine ya kwenye shughuli yetu ya leo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, nimekusikia.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kuweza kunipa fursa na mimi yakuweza kutoa mchango wangu mdogo katika hoja binafsi aliyoleta Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo napata mashaka na mashaka yangu kwamba sisi ndio watungaji wa sheria na sisi ndio wapitishaji wa sheria hizi. Lakini kwenye utekelezaji inakuwa ni mdogo sana, sasa hatujui ni kwa nini. Sheria nyingi tulizozipitisha hapa Barazani zinamtaka waziri husika awasilishe ripoti, lakini ripoti zile haziletwi sijui serikali inaukakasi gani ya kuzizuia ripoti zile kuletwa hapa. Juzi juzi katika Mswada wa Sheria ya Mafuta na Gesi ukiangalia ukurasa wa 80, kifungu cha 31(3) kinamtaka waziri husika awasilishe taarifa hapa, lakini pengine tutamaliza muda huu wetu sisi wa Baraza ripoti zile zisiletwe na Mhe. Dimwa, alisimama akasema kifungu kile cha 31(3) kiondolewe ili zile ripoti zisije huku zibaki huko huko wizarani, lakini serikali ikaji-*commit* kwa kifungu kile wacha kibakie ili hizi ripoti zipate kuletwa.

Vile vile, katika sheria hii ya fedha za umma, Sheria Nam. 12 ya 2005. Sheria hii vile vile inamtaka waziri husika awasilishe katika Baraza hili lako tukufu ripoti ya ukaguzi ya Mdhhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), lakini tokea ianzishwe sheria hii mwaka 2005 ripoti hii bado haijawasilishwa

Barazani na sheria ipo. Sasa ndio nasema sijui serikali ina ukakasi gani wa kuzileta ripoti hizi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashauri kwa vile sheria hii ya fedha inafanyiwa marekebisho kwa kufutwa kabisa na kuanzisha sheria nyengine mpya nimshauri Waziri wa Fedha na Mipango kwamba kile kifungu cha 36(4) ambacho ndio kinamtaka waziri husika awasilishe taarifa hii hapa Barazani basi katika ile sheria mpya kifutwe kisiletwe. Mimi hili nitalisimamia kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Fedha, Biashara na Kilimo, kwa hivyo na hili nitalisimamia kile kifutwe kwa sababu kukaguliwa anakaguliwa, lakini ripoti inabaki wizarani. Kwa hivyo, bora kile kipengele kisiwepo katika sheria hii ili hii ripoti isije kabisa, lakini kama kifungu hiki cha 36(4) kitaendelea kuwepo sisi Waheshimiwa Wawakilishi, tutauliza sana, tutahoji sana bila ya kupepesa macho na kwa hili Waheshimiwa Mawaziri mtustahamilie.

Mhe. Mwenyekiti, tusijenge mazingira ya mazoea kwamba ripoti hizi hazikuwasilishwa katika Baraza la Nane, hazikuwasilishwa katika Baraza la Saba basi mpaka hili Baraza la Tisa zisiwasilishwe, haiwezekani. Hili ni Baraza pekee Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Tisa ni Baraza la Tisa kweli kwani ni Baraza lenye viwango na kasi. Kwa nini nasema hivyo? Ni Baraza lenye viwango na kasi kwa muda mfupi kuna hoja binafsi 5 hazijawahi kutokea katika Baraza lolote, ndani ya kipindi cha miezi sita tuna hoja binafsi 5 tukimaliza miaka mitatu tutakuwa tuna hoja binafsi ngapi?Kwa hivyo, tunasema tusijenge mazoea hizi ripoti ziletwe, kama hazikuletwa basi sisi wawakilishi tutahoji kweli kweli.

Mhe. Mwenyekiti, moja katika misingi ya demokrasia na utawala bora ni msingi wa uwazi, sasa kama taarifa hizi haziletwi katika chombo hiki kitukufu na sheria zinataka ziletwe, huu msingi wa uwazi unatekelezwa vipi. Niiombe serikali isimamie vizuri msingi huu wa uwazi ili basi hizi taarifa huko zilikokwama zikwamuke na zije Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema sitaki kuchangia sana nimalizie kwamba tuhakikishe zile sheria ambazo tunazipitisha katika Baraza lako tukufu basi zinatekelezwa ipasavyo na zisitekelezwe nusu nusu, nyengine zinatekelezwa nyengine zinaachiwa. Baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Mihayo Juma Nh'hunga: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kupata fursa hii yakuweza kusema maneo yangu mawili, matatu, ama

kuchangia katika hoja hii iliyowasilishwa Barazani na Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa).

Kwanza kabisa kabla ya kumalizia niseme naunga mkono hoja kwa asilimia zote iliyotolewa na Mhe. Mjumbe, kama vile ambavyo dhamira yake ilikuwa inatuelekeza hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuchangia naomba niseme neno dogo, Baraza la Wawakilishi ni chombo pekee cha wananchi, lakini Baraza la Wawakilishi kupitia wawakilishi hawa ni *forum* pekee katika taifa hili ambalo linawakilisha mawazo ya wananchi waliokuwa wengi katika taifa lao. Sasa wakati mwengine serikali na taifa kwa ujumla inapokuwa na dhamira ya uanzishwaji wa mashirika ama taasisi hizi katika taifa inakuwa inadhamira njema kweli. Kwa hiyo, tunaipongeza sana serikali kuwa inaanzisha sheria na taasisi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mara nyingi uanzishwaji wa kitu unapoanzishwa halafu hatma yake kunakuwa hakuna ripoti inayojadiliwa kutokana na taasisi ile inapelekea watu kufanya kazi kwa mazoea. Mhe. Mwenyekiti, taifa letu lilipofika sipo kwa sababu taasisi nyingi, idara nyingi za serikali, mashirika mengi ya serikali tumekuwa na utaratibu wa kufanya kazi kwa mazoea.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nitaomba kuzungumzia hasa taasisi mbili, kwa mujibu wa sheria nianze na hii taasisi ya ZAECA kama ambavyo mjumbe muwasilishaji amelezea. Kwa mujibu wa sheria hii ya ZAECA ya 2012 katika *section* ya 12, tumetoa utaratibu kwa Mkurugenzi yule wa ZAECA kuwasilisha taarifa yake katika sehemu husika, kila inapofika mwisho wa mwaka wa bajeti ili dhamira na nia ya kuwasilishwa taarifa zake Barazani kujua ufanisi wa kazi zake kwa mwaka, kujua matumizi yake kwa mwaka, kujua mambo na changamoto zinazomkabili katika kila mwaka, kwamba taarifa ile itakapowasilishwa hapa Barazani Wajumbe watakaopata fursa ya kuchangia wataweza kutoa maelekezo yao pamoja na maboresho ili kuleta ufanisi katika taasisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha sana wakati mwengine taasisi zetu hizi zinapata changamoto kubwa sana katika utendaji wa kazi zake, lakini pale ikikosekana tu kutokuwasilishwa taarifa hii katika Baraza lako tukufu inapelekea taasisi zile kuvunjika moyo.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe mfano mdogo, katika Taasisi ya ZAECA ambayo mara nyingi inafanya kazi zake katika mazingira magumu sana, lakini

kutokuwasilisha ripoti yake katika Baraza hili inapelekea wananchi kutokujua nini kinafanywa na ZAECA. Wakati mwingine ugumu wanaoupata kutokana na ufanisi wao wa kazi ama utekelezaji wa majukumu yao kutokana na muingiliano wa idara mbali mbali za serikali unapelekea ugumu.

Mhe. Mwenyekiti, tuiombe sana serikali ni vyema ikafikia wakati ikaona haja ya msingi kwa utekelezaji wa sheria hizi ambazo chombo hiki na taifa hili kinatumia gharama kubwa, pesa nyingi za wananchi kwa dhamira ya kutunga sheria zilizokuwa bora na kuendesha mashirika yetu na taasisi. Sasa tuiombe sana serikali angalau ifanye jitihada sasa ya kuwasilisha taarifa zake katika chombo hiki cha wananchi kila mwaka kama ambavyo sheria imekuwa ikituongoza hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu waliopita kuchangia wamesema, lakini na mimi naomba nizungumze kidogo kuhusiana na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii imeanzishwa tangu mwaka 1964, kufikia mwaka 2014 imefikisha miaka 50 tangu uasisi wake, lakini jambo la kusikitisha kwamba ripoti za taasisi hii huwa hazijadiliwi. Msingi wa sheria ya taasisi hii umetokana katika Katiba yetu ya Zanzibar katika kifungu cha 112. Sasa inakuwa aibu na ajabu hata ule msingi wa Katiba yetu ambao tumeuweka kwa dhamira kuwa mashirika yetu haya ifike wakati taarifa zake zijadiliwe ili wananchi wapate kujua nini na nini kinafanyika katika taasisi hizi, ndio maana kila uchao wananchi wamekuwa hawaoni thamani na umuhimu wa kuwepo taasisi hizi katika taifa; inawezekana kinachofanyika na wanachokifanya kila mwaka kimekuwa hakionekani katika taifa hili.

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee kuiomba serikali, tuna imani serikali hii ni sikivu lakini jambo zuri zaidi katika kipindi hiki tunaamini katika taasisi hizi mbili ambazo nimezitaja zipo chini ya Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nina imani kwa serikali tuliyokuwanayo sasa tutaona haja katika Baraza hili la Tisa la pekee kuwasilisha taarifa hizi ili wananchi wapate kuziona, kuzielewa, kuzichangia na kutoa maoni yao; kurekebisha lakini hata kutoa mchango kwa dhamira ya kuleta maendeleo ama utendaji bora katika taasisi zetu hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie katika Mamlaka ya Maji (ZAWA). Utaratibu duniani kote na katika mataifa mengi linapoanzishwa shirika mara nyingi linakuwa na dhamira kuwa shirika lile liweze kujitegemea na sio kuitegemea serikali, lakini hapa kwetu mambo huwa ni tofauti, badala ya serikali kuweza

kutegemea shirika lile, lakini mara nyingi shirika lile linashindwa kujiendesha na kutegemea ruzuku kutoka serikalini kila siku.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, una dakika tatu.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Mwenyekiti, zitanitoshia sana hizo. Mhe. Mwenyekiti, sasa ifikie haja na wakati serikali ione thamani ya kuleta taarifa za mashirika haya katika chombo hiki kitukufu. Leo mamlaka inapata pesa nyingi kutoka serikalini, lakini wanachokifanya wananchi kwa ujumla wanakuwa hawajui shirika lile linafanya nini, ingawa kuna changamoto kubwa sana wanakabiliana nayo.

Sasa itafikia wakati Wazanzibari au wananchi wanahitaji kujua mashirika na taasisi hizi zinafanya nini katika taifa lao, lazima ufike wakati kila unapofika mwisho wa mwaka serikali ione umuhimu sasa wa taarifa hizi za mashirika haya kuweza kuwasilishwa katika chombo hiki kitukufu kwa dhamira ya wananchi kutaka kujua kinachoendelea katika taasisi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine serikali inatumia gharama kubwa sana na inapoteza fedha nyingi katika mashirika haya, lakini kutokana na kutokuwasilishwa tu kwa ile ripoti katika chombo hiki kitukufu mara nyengine watu wetu ama watendaji baadhi yao wana-*take an advantage* kwa dhamira ya kufanya yale ambayo wanajisikia ama kufanya kitu kwa mazoweza kwamba tutafanya hili, lakini ripoti hii haitoweza kwenda popote.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kuiomba sana serikali kuweza kuwasilisha ripoti zake hizi za mashirika haya. Baada ya hapo niseme naunga mkono hoja iliyotolewa na Mhe. Mohamed Said Mohamed, kwa asilimia mia moja. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said, lakini nakuomba sana Mheshimiwa pamoja na muda wako uende kwenye hoja ya msingi, muda haututoshi na muda wako ninakupa dakika kumi.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na nikushukuru kwa kuniita jina langu kwa usahihi kabisa, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze mtoa hoja kwa kuja kubuni, kuwaza, kukiri, lakini kwa lugha na maandishi ambayo ameyatumia, kwa utaalumu tunasema kwamba kwa lugha nyepesi kabisa, maana yake mtu yeyote akiisoma hii ripoti unaona kabisa Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mwakilishi wa

wananchi Jimbo la Mpendae kuwa ana hoja na kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizokuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitapenda nirudie yale ambayo tayari Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni aliyachangia kwa umakini kabisa na kuyataja mambo tofauti ambayo yanaendana na hoja hii. Kwa hiyo, muda wangu utakuwa ni mchache kabisa na nafikiri huo muda ulionipa pia sitazidi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme vitu viwili kwanza, hofu ninayoipata ni kwamba Kamati za Baraza la Wawakilishi zina wajibu wake kufanya kazi na katika suala hili zima hizi ripoti tangu tumeingia katika Mkutano huu, tumetoka katika Mkutano wa Bajeti na kuja sasa hivi hakuna eneo lolote jambo hili lililowahi kuzungumzwa juu ya ripoti. Ninaamini wawakilishi wengine wengi tuliokuwemo humu ambao ni wapya tumepatwa na mshangao kwamba kuna ripoti ambazo zinastahiki kuwa tuzipate. Kwa hiyo, mimi niombe serikali kutokana na hoja iliyoletwa inasubiri majibu, utekelezaji na ukiiona kabisa Waheshimiwa Mawaziri waliokuwa hapo mbele sasa hawana wasiwasi wameona hoja ipo, Mwanasheria Mkuu namuona kabisa kwamba yeye ametulia pale na hoja ameipokea.

Kwa hiyo, bila ya kupoteza muda mimi naomba vitu viwili; jambo la kwanza kwamba tupate majibu ni kwa nini haya mambo yamechukua muda mrefu. Hata kikao kilichopita katika Baraza lililopita Mhe. Mohamed Said Mohamed, amezungumza kwamba yeye alikuwa ni Mjumbe, lakini haya yote hayakuonekana.

Mhe. Mwenyekiti, baya zaidi ambalo limetajwa ni Ofisi ya Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Huyu ofisi yake imejigeuza kwamba ni kama ile ofisi ni mali yake mwenyewe, nimewahi kuzungumza nyuma juu ya maelezo anayozungumza na kwa utaratibu kama sijakosea ni zaidi ya miaka tisa huyu mtu ofisi yake haijakaguliwa na wala haitajwi. Pengine kuna umuhimu wa sheria kuziangukia upya, inawezekana kwamba serikali labda inamuogopa huyu ofisi yake ili kulinda maslahi ya pamoja, wote kwa pamoja, ndio maana ofisi ya CAG imekuwa haiguswi pamoja na mambo yote na kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizokuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa tayari hoja ni nzito, naamini hoja hii itafuatiliwa na serikali, serikali wapo wametulia na Mhe. Mwanasheria Mkuu, amesikia. Mimi niombe katika haya yote kwamba sasa tunakokwenda mbele huko kwa pesa na haya mashirika yote yametungwa kwa mujibu wa sheria basi utaratibu

uanze mara moja, kazi ianze kwenda mbele ili na sisi Wawakilishi wa wananchi tuweze kupata hizi taarifa ambazo ni muhimu.

Kama nilivyosema awali sitarudia yale ambayo yamechangiwa na hasa Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni amenifilisi kabisa yote ambayo nimeyakusudia.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii tena kumpongeza Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae kwa kubuni mawazo haya na kuja nayo na nimshukuru sana kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu ahsanteni sana kwa kunisikiliza, Mwenyezi Mungu awabariki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa sababu wachangiaji wamejitokeza na hoja haijafikia mwisho itabidi tumalize wakati wa jioni. Wachangiaji waliopo ni Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy na baadae Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hawa hatuna jinsi tutamalizia jioni, lakini pamoja na hayo naomba nitoe matangazo.

Kamati ya Ushindi ya *Simba Sports Club*, Wekundu wa Msimbazi wanatakiwa kukutana mara moja baada ya kuakhirishwa kikao hiki. Wajumbe wenyewe ni Mhe. Ali Salum Haji, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Shadya Mohamed Suleiman, Mhe. Abdalla Maulid Diwani, Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma na mratibu wa ushindi Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata). Hilo ni tangazo la Simba.

Tangazo jengine Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo wakitane katika ukumbi Nam. 3 baada ya kuakhirisha kikao hiki hivi sasa.

Tangazo la mwisho ni kwamba, Waheshimiwa Wajumbe kuna saa za ukutani zenye picha zenu wakati wa kuapishwa na Mhe. Spika pale, saa hizo zinazwa kwa bei nafuu nje ya *cafeteria* wote mnakaribishwa kwa kila mmoja kwenda kutizama picha hizo na kama zipo muweze kuzinunua. Ahsante.

Kwa kuwa muda uliobakia hatuwezi kuendelea tena naomba nichukue fursa hii kuakhirisha kikao hichi hadi saa 11:00 jioni kuendelea na hoja iliyopo mezani.

(Saa 5:47 mchana Kikao kiliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nina wajumbe wawili ambao watachangia baada ya hapo nitamwita Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, akifuatiwa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba na Sheria. Kwa hiyo, mchangiaji wetu wa mwanzo jioni hii Mhe. Panya Ali Abdalla, naomba uanze kuchangia.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe Spika, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi hii niweze kuzungumza machache juu ya hoja ya Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa). Awali ya yote nipende kutoa shukurani zangu za dhiti kabisa kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Dimwa, kwa hoja yake hii ambayo ameileta, ni kazi kubwa ambayo ameifanya mpaka kuweza kuleta hoja hii, kwa hiyo, anastahili sifa za pongezi kubwa.

Mhe. Spika, sisi ni wanaadamu na wanaadamu mapungufu ndio kazi yetu, kwa sababu ndivyo tulivyoubwa na Mwenyezi Mungu na ndio maana huwa kama sisi Waislamu basi huwa kina kitu tunajua kila inapofika wakati wa swala kila mmoja anaja wajibu wangu niende nikaswali. Lakini huwa kunawekwa Muadhini kwa sababu yakutukumbusha ili tuache shughuli tulizonazo twende kwa wakati ule tukashughulike na ibada. Kwa hiyo, kitendo alichokifanya Mhe. Mwakilishi, mimi namshukuru na nampongeza kwa sababu tumepitisha sheria nyingi hapa ambazo amezitaja katika hoja yake hii na zinaonekana hazijaweza kufanya kazi ili tukaweza kuwajibika vizuri katika sekta zetu. Kwa hiyo, kitendo alichokifanya hiki ni kutukumbusha sasa serikali zile sheria sisi ndio watungaji na wapitishaji, kwa hiyo, lazima wajibu uanze kwetu kuona tulichokitunga basi tunaweza kukifanyia kazi katika utekelezaji mzuri ili iweze kuleta ufanisi mzuri katika serikali yetu.

Mhe. Spika, niseme hoja hii ambayo ameileta Mhe. Mwakilishi, kwa kweli imetushtusha wajumbe, na mimi nimeshtuka sana pale nilipoona zile ripoti zote zinahusu mambo ya ukaguzi wa fedha ambao ndio unaotakiwa uletwe hapa, lakini ikawa imekosekana. Hiki ni kitendo ambacho kinaleta mshtuko kwa sababu mara nyingi wawakilishi tunapenda kuhoji mapato na matumizi ya serikali ili tuweze kujua vipi tulichokipata na vipi tumeweza kukitumia katika hali ya kuisaidia serikali iweze kufanya matumizi juu ya kuwapelekea huduma mbali mbali wananchi wake. Kwa hiyo, Mheshimiwa, ripoti hii imeonesha haya mapungufu ambayo yametushtusha kidogo kwa sababu taasisi zinaonekana kukosekana kuleta zile ripoti za ukaguzi au mapato na matumizi.

Hili si jambo zuri na mimi haja yangu niziombe zile taasisi husika ambazo Mhe. Mwakilishi, alizitaja katika hoja yake hii basi tuweze kupata majibu sahihi, kwa nini ripoti hizi zilikosekana na baada ya hapo labda kutokea hii hoja ambayo nimesema Mhe. Mwakilishi, amekuja kutukumbusha. Niseme sasa baada ya kupata haya serikali itakuwa imejipanga vipi kuhusu hoja hii iliyotokea yakukosekana hizi taarifa, ili taarifa hizi ni muhimu sana na hiki ndicho chombo cha wananchi ambacho wanakitegemea kwamba, sisi wawakilishi wao tumekuja hapa wanataka ripoti zao zote zitoke hapa kwa kusikia katika chombo hiki. Sasa serikali itwambie mpango na mkakati wake ambao imepanga baada ya kujitokeza hoja hii itafanya nini ili kuweza kujenga matumaini mema kwa wananchi wetu ambao hiki chombo ndio tegemeo lao.

Mhe. Spika, mimi sitaki kuchangia sana lakini nasema pia hoja hii inaweza kumsaidia sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kwa sababu yeye ndiye mwenye jukumu la kukusanya madughuli haya ili akaweza kuzipeleka katika serikali na serikali ikaweza kufanya matumizi yake kwa ajili ya wananchi wake kupelekea huduma mbali mbali. Sasa Mheshimiwa, fedha hizi au taarifa hizi zitakapofika katika Baraza hili zikasomwa na wawakilishi tukazisikia, ina maana tunaweza tukahoji pale patakapokuwa hapaonekani uhalali wa matumizi mazuri ya fedha za serikali tukaweza kuisaidia serikali, na tukaweza kumrahisishia mwenzetu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, ambaye anazisaka pesa kwa udi na uvumba ili serikali yetu hii iweze kujiendesha na kujikimu katika mahitaji mbali mbali.

Kwa hiyo, hii ripoti itaweza kumsaidia sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, sasa kuzitaka hizi taasisi isije ikawa kuna kivuli watu wamejificha kuficha zile ripoti kwa sababu pengine zinaonekana zina madudu fulani. Kwa hiyo, mimi Mheshimiwa, nilikuwa sitaki niseme mengi, nilitaka kusema machache lakini naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Mwakilishi, jambo ulilolifanya ni zuri na naamini serikali yetu ni serikali sikivu itaweza kuona kwamba pale ambapo tumesahau na tumepata mkumbushaji akatukumbusha, wanaweza wakafanya vizuri zaidi katika hoja hii na tukaweza kuisaidia serikali yetu, tukaweza kufanya kazi kwa ufanisi mzuri. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ahsante sana, kwanza kama kawaida tumshukuru Mwenyezi Mungu sote kutujaalia uzima na afya na hatimae leo tunatarajia kulifunga Baraza letu.

Mimi nina mchango wa kuchangia hoja hii ya Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa), hoja makini, hoja yenye ukweli na yenye utafiti wa hali

ya juu. Mhe. Spika, mimi nampongeza sana kwa sababu Waheshimiwa wenzangu kama hawa wanaopenda ukweli na kuweka mambo wazi wazi yanayotakikana katika jamii, mimi na-*support* asilimia mia kwa mia jambo hili kabla sijalichangia. Mhe. Spika, nitakwenda kwenye mchango huu halafu nitataka kupata majibu ya maswali ambayo nitayouliza.

Mhe. Spika, hapa kama ilivyoeleza hoja hii ina taasisi saba ambazo zinadhorota kuleta ripoti ndani ya Baraza la Wawakilishi. Mimi ningeomba sana kwanza hizi taasisi zingefahamu kwamba sisi wawakilishi tuliokuwemo humu ndani sote ni Zanzibar na Pemba kwa wananchi wote ndio tunaowakilisha. Kwa hiyo, tungeomba sana zinapotungwa sheria, zinapowekwa sheria katika Baraza hili la Wawakilishi basi zitekelezwe na ziheshimike.

Mhe. Spika, yale mambo yote yaliyokuwa yanatendeka, mimi naamini na nazungumza siku zote kwamba baadhi ya watendaji hasa hawa wanaotakiwa kufanya hizi kazi wanasababisha kuonekana serikali yetu na viongozi wetu wa juu waonekane kwamba hawafanyi kazi kumbe wao ndio wanaosababisha haya matatizo. Mimi ningeomba sana na namuomba sana Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Rais, mara nyengine wawachukulie hatua hawa, kwa sababu hali hii inawasababishia wao wenyewe waonekane kwamba kuna baadhi ya vitu wanaachiliwa, tukitake tusitake viongozi wetu ni wastaarabu tuliokuwa nao, na wana hekima.

Mhe. Spika, mimi ningetoa mfano mdogo tu, laiti watu hawa au taasisi hizi zingekuwa ziko kule *North* Korea na Venezuela na Cuba wangukuwa wameshanyongwa kwa haya mambo wanayoyafanya. Lakini kwa kuwa viongozi wetu wa nchi hii ni wastaarabu, wana imani wanawaachilia, ndio maana tunafika huku na haya mambo yataleta matatizo makubwa baadae, matokeo yake ndio hayo ndani ya nchi tuna majambazi, tuna mafisadi, tuna kila aina ya watu kwa sababu ya mambo kama hayo wanaogopa kuleta ripoti.

Hili mimi namuomba sana Mhe. Rais na Mhe. Makamu wa Rais, tunawatakia kila la kheri na najua watu fulani wachache tu ndani ya serikali nzima ndio wanaosababishia matatizo, kwa sababu yanapotokezea haya kwa vyovyote vile yanawagusa. Haya masuala ya utapeli wa maneno na kuja hapa kutuletea longo longo zimalizike, tunachotaka hapa ije ripoti kamili, tuelezwe kila kitu, tujadili tupate kuona nini tunasaidia, sio mambo yanafichwa fichwa tu.

Mhe. Spika, mambo haya mpaka lini tutaiweka serikali yetu ili iingie jina baya, tutakiweka chama chetu kionekane hakifati Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu ya watu watatu, wanne wanaosababisha serikali nzima na viongozi wetu

wa juu waonekane kwamba hawatendi haki. Mhe. Spika, mimi ningeomba sana kwanza kabla ya kuendelea kwa hawa waliochelewesha wote wachukuliwe hatua na waeleze vizuri kwa viongozi wahusika ili hivi vitu visurudie tena.

Mhe. Spika, mfano mdogo tu kwenye suala la *ZIPA* limetajwa humu ndani, hakuna ripoti yoyote ya *ZIPA* iliyokuja. Kuna *projects* zipo za Bakhresa kule Fumba, kuna *project* ya Manji ya hapo Bwawani, kuna *project* ya Bakhresa Mtoni, kuna *projects* ziko Matemwe, ziko *projects* karibu saba kubwa ambazo zina zaidi ya bilioni mia tano kila mtaji, lakini hakuna ripoti hata moja tuliyoletewa, hakuna tulichoelezwa, wananchi wanaona tu, sisi wenyewe hatufahamu matokeo yake ndio haya.

Kwa hiyo, tungeletewa ripoti ingekuwa tushafahamu na wananchi wote wameshafahamu nini kinafanyika ndani ya nchi. Haya yote ni matatizo ya kwamba hizi taarifa hiziji, mfano mdogo hii taasisi ya kudhibiti mahesabu ya serikali ilitaka kipindi cha nyuma ikafanye ukaguzi wa *Airport* ikapeleka ripoti inataka milioni 35 ikafanye uchunguzi basi ilipewa milioni tano. Hivi kweli *Airport* nzima kwenda kufanya uchunguzi na wataalamu kuona hasara zilizotumika na fedha zilizotumika nyingi milioni tano itaweza wapi, matokeo yake imewakwamisha na haya ndio mambo ambayo yanayosababisha kwamba ripoti zisije. Mimi ningeomba sana serikali ichukulie mkazo na iheshimu Baraza la Wawakilishi, watendaji wote watulettee ili tuweze kuyajadili haya mambo na tuyaone.

Mhe. Spika, vile vile, ningeenda kwenye suala la kutaka kujua *tax holidays* hizi kuna *exemption*, kuna watu wanapewa na wafanyabiashara wakubwa wakubwa ma-*investors*, ma-*exemption* hatujui, tulikuwa tuje tuelezwe tu safari hii misamaha iko hivi, iko hivi. Mimi kwanza nampongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kwa kuanza kuondosha watu ambao wamesababisha hasara ndani ya serikali, nampongeza sana kwa hili. Najua akianza hivyo atapata maadui tu na naomba sana mawaziri wenzake wanao watu kama hao na wao wajitokeze wasimuachie yeye peke yake, wasione tabu, wamuige kwa wale wote wanaohusika, sio mtu yeyote tu, kama alivyofanya yeye wanaohujumu uchumi, wanaotia serikali jina baya pamoja na viongozi wetu, wanaokitenda Chama cha Mapinduzi vibaya wafukuzwe na wachukuliwe hatua. Mawaziri wengine mpaka leo wamekaa tu huko mbele hawajamtoa mtu yeyote, hawajafanya lolote, wanamuachia mwenzao tayari ameshaanza kazi.

Kwa hiyo, ningeomba sana wafanye uchunguzi kwani uzembe ushafanyika, tumeshaona taasisi saba zaidi ya miaka kumi hazijaleta ripoti na hakuna yoyote iliyochukuliwa. Kwa hiyo, tunaomba sana mawaziri wengine igeni

mfano wa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kuwaondosha wale wote wanaoleta uzembe na wale wote wanaoharibu fedha za serikali na za wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, hapa kawaida ya nchi yetu unapozungumza ukweli na unapoleta hoja kama ya Mhe. Mohammed Said Mohammed, hoja makini matokeo yake ataanza kuambiwa katumwa, *CUF*, sijui nini, kumbe humu ndani kuna balaa zaidi. Sisi tunachotaka ni ukweli, hapa tupo kwenye kutengeneza ukweli, hatuogopi mtu na Mwenyezi Mungu ndiye aliyetuumba kwenye ukweli tutazungumza ukweli, na la kuitetea serikali tutalitetea na yule atakayekwenda kinyume tutamtaja humu humu ndani. Mhe. Spika, mimi nampongeza sana kwa sababu tabia hizi zipo, likizungumzwa la ukweli tu watu weshatafsiri vyengine nje.

Mhe. Spika, kuhusu Mamlaka ya Maji, maji kila siku matatizo, kuna miradi mikubwa mikubwa. Miradi ya *ADB*, *JAICA*, Ras al Khaima, hakuna hata siku moja ripoti iliyokuja wakati ma-*billion of shillings* yanatumika ndani ya nchi. Kwa hiyo, tungeomba sana hizi ripoti zije kamili, ziletwe na waziri utueleze kinaga ubaga usitufiche hata jambo moja. Sisi wawakilishi wa Baraza la Tisa la safari hii hatutaki longo longo, hatutaki utapeli wa maneno wala kwa vitendo, tunafuatilia na tuko makini, tukija tukamkamata mtu yeyote anatudanganya tutamuweka hadharani.

Mhe. Spika, na mimi binafsi Mwakilishi wa Jimbo la Chaani nazipa onyo sana hivi taasisi zilizokuwa hazijaleta zituletee, zifate sheria, zisivunje sheria, sisi ndio tunaotunga sheria na sisi tunawawakilisha wananchi wote milioni mbili na nusu wa Zanzibar na Pemba wanataka kujua nini tufanya, tukiendelea hivi kila siku itakuwa hatufiki. Vile vile, nampongeza Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nampongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, kwa utendaji wao mzuri na hekima zao, lakini nawaomba sana mara moja moja wageuke kama yule wa *North Korea* awaadhibu hawa.

Hizi nchi tunazona, watu hawaachiliwi, unajua tuzungumze ukweli viongozi wetu ni wastaarabu na ndio maana tunafika huku, laiti kama tutakuwa siku moja tuko wakali tuwatie adabu wataharibu nchi, wanaitia serikali jina baya na wao waheshimiwa wetu wakubwa tunawaheshimu wanaingizwa jina baya kwa watu wanne, watano. Hili suala limalizike na Baraza la Tisa safari hii tutahakikisha kwamba hawa watu wote wanaoleta mambo haya wataondoka, tutashindwa sisi au watashindwa wao, hilo ndio moja tutalolijua safari hii. Mhe.

Spika, mimi naishia hapa hoja naikubali asilimia mbili niko nayo pamoja. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama nilivyosema hao ndio walikuwa wachangiaji wetu wa mwisho, lakini sasa nitawaita wachangiaji watatu, nitaanza na Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, halafu atafuatiwa na Mhe. Waziri wa Fedha, baadae atakuja kumalizia Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Mhe. Waziri wa Maji karibu sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na mimi naomba nichangie hoja hii kama ifuatavyo.

Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hapa jioni hii wakati tunamalizia kikao chetu cha Baraza, lakini naomba niseme kwamba serikali iko makini sana katika kutekeleza majukumu yake na kila nikiangalia serikali hii naona kama ni serikali shirikishi, ni serikali ambayo wakati wote iko katika kufuata sheria na utaratibu. Lakini nilikuwa najiuliza toka asubuhi nikawa naisoma hii *paper* kuna mambo nilikuwa najiuliza, bahati mbaya sana mimi ndio mara yangu ya kwanza kuingia ndani ya Barazani, lakini uzoefu niliokuwa nauona nilikuwa msikilizaji mzuri ndani ya Baraza.

Lakini huko nyuma sikuona ila nikasema hapa nini kimekosewa lazima tujiulize, nilivyokuwa nakiangalia nikasema utaratibu mzima inaonekana hata ndani ya Baraza letu sisi kama watunga sheria tulikuwa bado hatukuwa makini katika hili. Lazima tukiri kwamba hatukuwa makini, kwa hiyo, ni vyema kwa sasa hivi basi tuwe na utaratibu mzuri kwa sababu na mimi pia nilijaribu kupitia sheria nyingi nyingi baada ya kuona Mhe. Mohammed Said, wakati ule alipokuwa akiniambia. Mimi wakati wanazungumza ripoti nikajua ni ripoti ambayo inawasilishwa wakati wa bajeti, lakini baadae akaniambia hapana. Sasa kama hivyo ndivyo maana yake nini? Utaratibu mzima wa kwenye Baraza lazima tujue ni wakati gani na lini ripoti hizi zinataka kuwasilishwa.

Tunasema tunawasilisha lakini je, tunapata fursa ya kuingia Barazani na kujiadili ripoti, kwa sababu sijaona hizo ratiba. Sasa kama zipo basi nafikiri sote kwa pamoja tujipange katika hili kwamba, Baraza hili la siku 10 ni Baraza la kujadili ripoti za mawizara, Baraza hili ni kwa ajili ya kujadili bajeti. Sasa mimi nafikiri ni umakini wa kuweka utaratibu mzuri wa kuweza sisi sote kufikia hilo ambalo tumekusudia, kwa sababu sheria hizi kila nikiangalia tunatunga sisi, na wengine bahati nzuri wako kwa muda wingi na wengine walikuwa viongozi, lakini hatukuliona hili. Kwa hiyo, ndio maana nikasema basi bora nisimame umakini wetu kwa pamoja ndio utatafikisha hapa, lakini

vyenginevyo tukisema tu serikali, serikali ni pamoja na sisi kwamba, sote tutakiwa kusimamia sheria lakini sote tunataka kujua wajibu kila mtu ajue wajibu wake ni nini, sisi hapa tuko on *behalf* ya wananchi wetu na sheria tunawatungia sisi on *behalf* ya wao.

Kwa hiyo, na utekelezaji wake pia unahitaji hivyo hivyo Mhe. Spika. Kwa hiyo, mimi niombe sana Baraza lako tukufu kupitia watendaji wako makini, lakini pia kupitia Wajumbe wa Baraza hili sasa tuanze utaratibu mpya ambao ulikuwa haupo, maana yake ilikuwa sijauona awali ulikuwa haupo basi tuanze utaratibu mpya ambao tuwe tuna *session* ya kujadili ripoti. Serikali haina shida wala haina tatizo, serikali ipo kwa sababu ya kutekeleza majukumu yake na kuhakikisha kwamba wanalinda sheria zilizopo.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia hoja iliyotolewa na Mhe. Mwakilishi, kuhusu ukiukwaji wa sheria wa baadhi taasisi ambazo zinazotakiwa kuwasilisha taarifa zake mbele ya Baraza hili.

Kwanza Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi, kwa kuwasilisha hoja hii muhimu. Ninamshukuru kwa kuibua kitu ambacho kwa kweli kitatusaidia. Mhe. Spika, hii ni hoja ya kujenga ambayo inahimiza uwazi na uwajibikaji. Na tumshukuru kwa hilo lakini vile vile nichangie mambo mawili, matatu ambayo nitaomba sana Mhe. Spika, kwa Mhe. Mwakilishi na Waheshimiwa Wajumbe, walizingatie hili. (*Makofi*)

Kwanza tutofautishe kwamba tuna mashirika ambayo hii ndiyo mitaji ya umma. Mashirika haya yamesajiliwa kwa Sheria ya *Public Investment Act* ya 2002 na yapo yana orodha yake. Yapo yale ambayo yanaendeshwa kibiashara. Kwa mfano *Zanzibar Shipping Co-operation, ZECO, ZSTC, Zanzibar Insurance Company. PBZ* imejisaliwa kama kampuni, lakini nayo inaweza kuingia kwenye mitaji ya umma. (*Makofi*)

Lakini vile vile yapo mashirika yaliyosajiliwa kwenye Sheria hii lakini ni ya huduma ambayo ni *Zanzibar Leo, ZBC* na Shirika la Maktaba. Vile vile, tutofautishe na Wakala wa Serikali (*Agency*) na taasisi nyengine. Sasa hizi *agencies* na taasisi nyengine yapo ambayo yamesajiliwa kwa Sheria za kuanzishwa kwa *agencies* hizo au taasisi hizo. Na sasa hivi zina sheria zake na zipo zilizoelekeza kwamba zile taarifa zao ziwasilishwe katika Baraza la Wawakilishi.

Nikitoa mfano, kwenye ukurasa wa 2 wa taarifa ya Mhe. Mwakilishi. Kwenye Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (ZIPA), hii imesajiliwa kwa Sheria ya ZIPA Nam. 11 ya 2004 ambayo sheria hii kwa bahati haina *requirement* hiyo ya kwamba taarifa ziwasilishwe kwenye Baraza la Wawakilishi. Na zipo vile vile taasisi nyengine ambazo hakuna *requirements*. Lakini pia la msingi tuzingatie kwamba kwa mashirika hasa mashirika ya umma, hizi ni *non-portage* na utaratibu wake haupitii kwenye *Appropriation Bill* kwa maana ya zile bajeti zao. Zina utaratibu mwingine wa Bodi kupitisha na Waziri kuidhinisha.

Sasa hivi kwanza tuzitofautishe kwa sababu humu kwenye taarifa zimechanganya sana, ili tuzijue zile taasisi ambazo zina *requirements* ya kisheria ya kwamba taarifa zao ziliwasilishwe hapa. Lakini haya mashirika ambayo yana-*requirements* kwa Sheria hii ya Mitaji ya Umma ambayo *section*, ninadhani kwenye *section* ya 27, kweli kabisa inatamka wazi wazi kwamba taarifa zao ziwasilishwe katika Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Sasa kuwasilishwa taarifa zinawasilishwa. Kupitia kwenye taarifa ya CAG mashirika yote haya hesabu zake zinawasilishwa kwenye Baraza la Wawakilishi. Lakini hiyo haitengui ile Sheria ambayo inataka kweli kweli Waziri anayehusika na Taasisi ile au Shirika lile kuwasilisha taarifa yake mapema. Kwa hivyo, hilo sisi tunalichukua. Mhe. Mwakilishi, ameliona tunalichukua. Taarifa zinawasilishwa lakini pengine utaratibu haukuzingatia matakwa ya kisheria. Hivyo, hilo tunalichukua. (*Makofi*)

Lakini tutofautishe zipo wakala wa Serikali (*Government Agencies*) na taasisi nyengine ambazo zimetajwa humu, lakini ukizipitia sheria zake hazina *requirements* ya kisheria ya kwamba taarifa hizo ziwasilishwe kwenye Baraza hili. Kwa hivyo, nilitaka Mheshimiwa, alifahamu lakini kwa zile ambazo zina *requirements*, sisi tunachukua na tutazifanyia kazi. (*Makofi*)

Lakini niseme tu Sheria hii ya *Public Investment Act* ya 2002, nayo ina mapungufu yake. Kwa sababu ndani ya kile kifungu cha *section* ya 27, iliyotaka taarifa za mashirika hayo kuwasilishwa hapa. Kwa bahati mbaya ipo wazi, haikutoa muda, ilikuwa inasema tu, "*Soon after receiving report*", Waziri atawasilisha taarifa ile katika Baraza la Wawakilishi. Lakini *soon*, *how soon it is*, haikuwa-*specified*.

Sasa sisi Mhe. Spika, tunaifanyia mapitio sheria hiyo, baada ya kugundua mapungufu mengi, tunaifanyia mapitio na tayari tumeshafungua *tender*, hivi sasa inafanyiwa tathmini na itafanyiwa kazi chini ya mradi wa *Public Finance Management Reform Programme* ambayo ina ufadhili na fedha zake zipo.

Katika kuifanyia mapitio sheria hiyo, kuna mambo ya msingi ambayo itabidi tuyazingatie. Moja sisi tutazingatia kama pendekezo la kuanzishwa *An independent Authority* ya kusimamia mashirika haya. Na hili si jambo geni kwa sababu wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari wana Ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo kazi yake ni *specifically* kabisa kusimamia mashirika. (*Makofi*)

Sasa hilo linaweza likaja kama pendekezo na likiridhiwa na Serikali na Baraza la Wawakilishi, si lazima tuwe na kitu kama hicho, lakini tutakuwa na chombo ambacho kitaweza kusimamia kwa karibu zaidi utendaji wa mashirika hayo. Serikali imefanya juhudi kubwa sana katika kuimarisha mashirika haya na niseme hivi sasa mashirika haya yanafanya faida. Mengi yao yanafanya faida lakini pia na Serikali imekuwa ikipata sasa gawio lake kutokana na faida hiyo.

Kwa mwaka wa fedha uliopita yaliweza kuchangia karibu milioni mia saba na yangeliweza kuchangia karibu bilioni tatu kama *PBZ* nayo isingekuwa na masharti ya ziada ya *BoT* iliyozuiwa kutoa gawio lile. Kwa hivyo, sasa kiufanisi yanakwenda vizuri, mengi ya mashirika hayo baada ya kufanyiwa kazi kubwa sana na Serikali. Sasa niseme tu na niwaambie Waheshimiwa Wajumbe, kwamba Serikali imeichukua hiyo *observation* ya Mhe. Mohamed Said Mohamed, wajibu wa kisheria kwa yale mashirika na taasisi zinazopaswa kisheria kuwasilisha taarifa zao Barazani, hilo tutalichukua. Lakini bado nimueleze kwamba Serikali inafanya juhudi kubwa sana ya kujengea uwezo hasa wa kitaaluma watendaji wa mashirika haya ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi na mashirika yetu haya yaende kibiashara na yawe na tija na yachangie katika uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tunajaribu pale Wizara ya Fedha na siyo kujaribu lakini tunafanya kweli kweli kujengea uwezo Idara yetu inayosimamia mitaji ya umma. Kwanza kwa kuongeza idadi ya wafanyakazi, kwa sababu wafanyakazi waliopo pale hawatoshi kusimamia mashirika yetu. (*Makofi*)

Lakini la pili wale wafanyakazi wanaoisimamia mashirika haya lazima wajengewe uwezo wa kitaaluma wa kuweza kufanya kazi ya usimamizi na ufuatiliaji. Hiyo kazi inafanyika na tutafanya tathmini ya kina kwa mashirika yetu haya ili kuona kweli yanakwenda kibiashara kama azma ya Serikali ilivyokusudia.

Mhe. Spika, niliomba kuchangia hayo kutoa ufafanuzi huo na nirudie tu kwamba siyo yote yaliyoorodheshwa humu tuyafuatilie kwa mujibu wa sheria

zao, yanapaswa kuwasilisha taarifa hizo katika Baraza hili. Lakini yale yanayopaswa tutayachukua. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri na Mipango. Sasa nimwite mchangiaji wa mwisho wa hoja hii Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Karibu sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru na nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi alaasiri hii kupata nafasi ya kueleza mambo fulani fulani.

Hoja hii ya Mhe. Mohamed Said Mohamed, imechangiwa karibu na karibu Waheshimimiwa wanane na mimi nitakuwa nitakuwa wa tisa. Nao:-

1. Mhe. Omar Seif Abeid
2. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
3. Mhe. Mihayo Juma N'hunga
4. Mhe. Simai Mohamed Said
5. Mhe. Panya Ali Abdalla
6. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
7. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
8. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango
9. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Spika, mimi kwanza nichukue nafasi hii nimshukuru sana sana Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae Mhe. Mohamed Said Mohamed. Ninadhani kuna siku mtu ameniambia huyu Mhe. Mohamed Said Mohamed, ni *doctor*? Nikamwambia ni *doctor*, kwani *doctor* lazima awe anapiga sindano tu. Kwa sababu *doctor* anaweza kuwa *doctor* kama una utaalumu fulani, ni *doctor* vile vile, ukawa unatibu watu kama vile mwalimu. Mwalimu siyo lazima upitie *teacher training*, kile utakachomfundisha mtu na akakifahamu basi wewe ni mwalimu, chochote. Kwa hivyo, sote ni walimu humu. (*Makofi*)

Mhe. Mohamed Said Mohamed, leo amefanya jambo zuri sana ametupa taaluma ya kutukumbusha. Kwa hivyo, nimshukuru yeye kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba Sheikhe Mohamed Said Mohamed, amefanya kazi nzuri sana leo. Mhe. Panya Ali Abdalla, kasema, sala Waislamu tumehimizwa tusali sala

tano, lakini Alfajiri adhana ya kwanza inapigwa ya kuhimizwa tayari mambo ya sala imeshafika, baadae kama baada ya nusu saa au saa kasobo inapigwa wenyewe sasa adhana, kwamba sasa sala imeshaingia na mambo mengineyo. Ikifika Adhuhuri hivyo hivyo, Laasiri, Magharibi na Insha. Kwa hivyo, alichofanya Mhe. Mohamed Said Mohamed, si kitu kigeni kipo. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed Waziri wa Fedha na Mipango, kasema kakiibua. Na kweli kapiga mbizi na sioni ajabu kwa sababu huyu ni mtu alikuwa Wizara ya Uvuvi vile vile anajua kupiga mbizi huyu. (*Makofi*)

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nimshukuru sana. Lakini kimsingi Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed, ametueleza vizuri sana, ametoa ufafanuzi mzuri sana. Mimi nikiri kwamba kuna makosa au kuna *short coming* katika ripoti hizi. Kama alivyoeleza ni sahihi lakini ninapenda niwaahidi Waheshimiwa wote kwamba Mhe. Spika, mbele yako kwamba Serikali ya Awamu ya Saba ina nia nzuri kabisa na azimia na inaendeleza kuimarisha utawala bora. Na utawala bora ni hii kuwa na uwazi na ukweli. Ikifika taarifa hapa Mhe. Spika, Waheshimiwa hawa, jana nilisema hapa sikutania, Waheshimiwa hawa michango yao ni mizito na kila anayesimama na kila mmoja kazungumza kwa uchungu, kazungumza kwa nia nzuri kabisa ya kutaka kusaidia. (*Makofi*)

Kwa hivyo, michango hii ni mizuri inayochangiwa hapa na wote wamezungumza nia hiyo hiyo kwamba tunataka ziletwe hapa tujiridhishe, kwa sababu zile ni pesa za umma, pesa za wananchi tunahitajia kujijua namna zinavyotumiwa, zinavyopatikana tuelezwe na zinavyotumiwa vile vile. Tusiwe mahodari wa kukusanya tu, lakini tuwe mahodari wa kutoa taarifa namna tunavyozitumia. (*Makofi*)

Hivyo, Serikali ya Awamu ya Saba imedhamiria kuimarisha utawala bora kuhakikisha kwamba vyombo vyote vya umma ambavyo vinatumia raslimali za umma, vinafanya kazi kwa mujibu wa sheria zinazoongozwa na taasisi hizo. Lazima kuwe kuna sheria zinazoongoza taasisi hizo na zifanye kazi kwa mujibu wa sheria hizo.

Aidh, Serikali itahakikisha kwamba taarifa za kila taasisi ambazo zinawajibika, ninarudia tena hapa, kila taasisi ambazo zinawajibika kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa sheria zinazoongoza taasisi hizo, zinawasilisha katika Baraza la Wawakilishi kwa wakati na kwa ukamilifu, ili kulipa nafasi Baraza la Wawakilishi lako Tukufu Mhe. Spika, kuchangia taarifa hizo kwa lengo la kuimarisha utendaji wa taasisi zetu. (*Makofi*)

Kwa hivyo, mimi ninaahidi kwa niaba ya Serikali, kama ninayesimamia masuala ya utawala bora nitahakikisha kuwa hilo tunalisimamia na tunawakumbusha Mawaziri wote ili kuhakikisha taarifa hizo zinaletwa kwa wakati na kwa utaratibu unaofaa. Na moja ambalo ninataka nitoe taarifa Mhe. Spika, watu wamezungumzia sana tokea wakati wa bajeti yangu ya Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wao walisema sana kwamba CAG naye akaguliwe. Kwa sababu yeye anakagua wenzake, yeye hajakaguliwa. (*Makofi*)

Katika bajeti yetu ya mwaka huu ya 2016/2017 ninaahidi kwamba CAG atakaguliwa na taarifa yake italetwa hapa. Na wala tusiwe na mashaka Mhe. Spika, taarifa ya CAG itakaguliwa. Tunafanya taratibu sasa hivi ya kutafuta, tumwite nani yule, tumwite *contractor* au tumwite sijui nani, mkandarasi atakayeweza kututafutia akatutafutia utaratibu mzuri.

Tutatoa *tender* Mhe. Spika, ili atakayeweza kufanya kazi yote tukathibitisha na kwa mujibu wa mamlaka, Waziri ndiye anayeteuwa muhusika yule, atakwenda kukaguliwa na taarifa zitaletwa hapa. Hivyo, tutulieni Serikali hii ya Awamu ya Saba inayongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, ni makini na musiwe na wasi wasi, mambo yatawekwa hadharani hapa kwa kila kitu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi ninampongeza sana ndugu yangu Mhe. Mohamed Said Mohamed, ninampongeza sana kwa kuibua huko alikokwenda chini akapiga mbizi akatoa vitu alivyotoa. Lakini kama alivyosema Mhe. Dkt. Khalid Salum, ni kweli kuna baadhi ya mashirika haya yameundwa kwa sheria zao. Kitakachofanyika sasa hivi ni kuziangalia sheria zote zile za mashirika pamoja na sheria zetu hizi ambazo zinaongoza katika kuleta taarifa hizi hapa kwamba zinazoeleza kuwa taarifa hizi ziletwe hapa, tuziangalie na tuseme hazina mgongano ili tuweze kuweka sawa mambo hadharani na tuyalete hapa Barazani yajadiliwe. (*Makofi*)

Baada ya hayo Mhe. Spika, mimi naomba kuwasilisha na ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ninawatakia kila la kheri Waheshimiwa, mapumziko mazuri baada ya kuahirishwa Kikao hichi.

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Sasa naomba nimwite mtoa hoja Mhe. Mohamed Said Mohamed, ili aje ahitimishe hoja yake. Karibu sana Mheshimiwa.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa imani yako kwa kuniita jioni hii ya leo na mimi nikaweza kuhitimisho hoja yangu ambayo nimeileta ndani ya Baraza la Wawakilishi ya Ukiukwaji wa Baadhi ya Sheria Mbali Mbali na Taasisi zake.

Mhe. Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu hii, kwanza ningekuomba sana unipe muda dakika moja au sekunde thalathini ili sasa niipongeze ile Kamati ya Ushindi ya Yanga. Kamati hiyo ambayo Mjumbe wake ni Issa Haji Ussi (Gavu), Haji Omar Kheir, Miraji Hassan Mussa na Mhe. Mohamed Said Mohamed, pamoja na mtendaji wetu Dau Hamad Maulid. (*Makofi*)

Niseme tu ushindi upo musiwewe na wasi wasi.

Mhe. Spika, sasa naomba niweze kuhitimisha hoja yangu hii. Kwanza, niweze kuwatambua wale wote ambao wamechangia kwa njia moja au nyengine hoja yangu hii. Nao ni:-

1. Mhe. Omar Seif Abeid
2. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
3. Mhe. Mihayo Juma N'hunga
4. Mhe. Simai Mohamed Said
5. Mhe. Panya Ali Abdalla
6. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
7. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
8. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango
9. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Spika, yote waliyochangia yalikuwa yana maana ya kuweza kutukumbusha lakini vile vile walikuwa na maana kubwa ya kujenga.

Mhe. Spika, wengi walikwenda kwenye taasisi ya Mamlaka ya Maji ambayo Mhe. Nadir Abdul-Latif, alisema kuna miradi mingi ambayo imetoka lakini maji yamekuwa tatizo. Lakini nasema tu Waheshimiwa Mawaziri wapo na wao wameshalichukua. Kwa sababu hiyo basi Mhe. Nadir, alisema kuna *operation cost* ambayo ni milioni 400 ambayo inaweza kwenda na Mamlaka ya Maji, lakini *income cost* ni milioni 2, kwa hivyo, kuna tofauti kubwa. Sasa kitu kama hiki ni vyema kama tunaleta ripoti zetu hapa wananchi wanaweza kuvichangia kwa umuhimu zaidi.

Mhe. Spika, nilisahau kwa sababu mmoja aliniletea kwa maandishi ni Mhe. Rashid Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, yeye aliniletea kwa maandishi, namshukuru kwa kuchangia hoja yangu hiyo na kuikubali kwa asilimia mia.

Mhe. Spika, wengi waliokwenda wamekwenda kutukumbusha, lakini wengi wamezungumzia taasisi mbali mbali ikiwa mamlaka ya viwanja vya ndege, na vyenginevyo. Lakini niseme tu kuwa nakubaliana na hayo yote ambayo waheshimiwa wameyataja hapa. Lakini kubwa zaidi niseme kwa sababu Rais wetu sio mwanasheria, ndio sababu sasa, lakini yeye pia hayuko juu ya sheria, ametumia kifungu namba 55 kumchagua Mhe. Mwanasheria Mkuu. Mwanasheria Mkuu kazi zake zipo katika kifungu cha 56 na tunazielewa. Mimi nakubaliana naye Mhe. Mwanasheria Mkuu, ni mkomavu wa kisheria, lakini ni msomi mzuri katika wasomi wa Zanzibar wa sheria, lakini cha kusikitisha na cha ajabu kubwa, Mwanasheria Mkuu ameshindwa kuishauri serikali juu ya kuleta hoja hizi hapa. (*Makofi*)

Pia, Mhe. Rais, amemteua Mhe. Haroun Ali Suleiman, kwa kifungu namba 42 kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Haroun Ali, ninavyomuelewa ni mwalimu wangu, lakini kama ni mapendekezo yangu kwa utumishi wake uliotukuka, chuo chochote kikuu cha Zanzibar au kwengineko duniani, inapaswa apewe udaktari wa heshima. Kwa kazi zake kubwa kwa kipindi cha miaka 20 katika Baraza hili, hakuna asiyemjua kwamba amefanyakazi za umahiri mkubwa na vile hajawaji kushindwa kazi ambayo amepewa. Lakini cha kusikitisha sana, waziri mkongwe kama yeye ameshindwa kabisa na yeye kuishauri serikali. (*Makofi*)

Pia, Rais ametumia kifungu cha 47 kumteua msomi mwingine wa juu wa sheria, ndugu yangu Naibu Waziri Khamis Juma Maalim na yeye ni mwanasheria, ni msomi mzuri tu, lakini na yeye ameshindwa kumshauri Rais au kuishauri serikali kuleta hapa. (*Makofi*)

Lakini vile vile Mhe. Rais, amemteua tena Naibu Katibu Mkuu Mashaka Kubingwa Simba, ni mwanasheria vile vile mzoefu, lakini wote wameshindwa kutumia haki yao ya kuishauri serikali kuleta ripoti hapa.

Mhe. Spika, nilikuwa nioneshe hiyo moja kwa sababu wote Maalim Haroun Ali Suleiman ni mwalimu wangu, lakini AG ni rafiki yangu mkubwa sana. Mhe. Spika, baada ya dibaji hiyo na baada ya maelezo ya hoja yangu, naliomba Baraza lako tukufu sasa liazimie mambo mawili kama ifuatavyo;

Moja, serikali iandae utaratibu maalum ili kuhakikisha kuwa taarifa zote ambazo zinatakiwa kuwasilishwa mbele ya Baraza kwa mujibu wa sheria, zivasilishwe kwa wakati na kwa mujibu wa sheria hii. (*Makofi*)

Mhe. Spika, jambo la pili, serikali ifanye marekebisho ya sheria kwa mashirika au taasisi zote, ambazo hazipaswi kwa mujibu wa sheria, kuwasilisha taarifa zake mbele ya Baraza lako tukufu, ili sasa zivasilishwe mbele ya Baraza. Kwa mfano, Mashirika ya Bandari na mashirika mengine itakavyoonekana sheria inafaa.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache na muhitimisho wa taarifa yangu hii, sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wajumbe, hoja binafsi ya Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) imetolewa, na imeungwa mkono na waliowengi. Sasa naomba niwahoji wanaounga mkono azimio hili pamoja na maazimio yake wanyanyuwe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Kwa hivyo, nadhani kuwa tunakubaliana kwamba madhali imeshapita, sasa serikali ichukuwe hiyo hoja pamoja na yale maazimio ili serikali waweze kuyafanyiakazi. Katibu kwa shughuli zinazoendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ushahidi Sura ya Tano na Kuandika Sheria Mpya ya Ushahidi na mambo mengine yanayohusiana na hayo

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ushahidi Sura ya Tano na Kuandika Sheria Mpya ya Ushahidi na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, naomba nimwite Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, ili na yeye aje awasilishe miswada naona mitatu. Karibu sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Ni kuisoma kwa mara ya kwanza, ndio.

**Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko
wa Hifadhi ya Jamii namba 2 ya mwaka 2005**

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii namba 2 ya mwaka 2005, kuweka masharti bora zaidi, kwa ajili ya ufanisi na usimamizi imara wa mfuko na mambo yanayohusiana na hayo. Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Mhe. Spika: Ahsante, mswada unaofuata.

**Mswada wa Sheria Kutunga Sheria ya Usimamizi wa
Fedha za Umma na Kuweka Masharti Bora ya
Kudhibiti na Kusimamia Fedha za Umma**

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria Kutunga Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kuweka Masharti Bora ya Kudhibiti na Kusimamia Fedha za Umma, na kuweka mambo mengine yanayohusiana na hayo, na Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Serikali namba 12 ya mwaka 2005. Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na mswada wa mwisho ambao unauwasilisha.

**Mswada wa Sheria Kufuta Sheria ya Ununuzi na Uuzaji
wa Mali za Serikali namba 9 ya mwaka 2005**

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria Kufuta Sheria ya Ununuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali namba 9 ya mwaka 2005, na Kutungwa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Ununuzi na Uuzaji wa Mali za Umma na Kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo. Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, naona kulikuwa kuna hoja. Asubuhi ile miswada ilikuwa inawekwa mezani, sasa hivi ndio inasomwa kwa mara ya kwanza. Kwa hivyo, utaratibu unaofuata uko sahihi tu.

Waheshimiwa Wajumbe, shughuli zote ambazo tumezipanga kwa ajili ya mkutano huu ndio zimeshamalizika rasmi. Sasa kabla sijamkaribisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, aje atowe hoja ya kuahirisha Baraza, naomba nichukuwe nafasi hii Waheshimiwa Wajumbe, kuwapeni shukrani zangu za dhati sana, kwa mashirikiano ambayo tulikuwa nayo katika kipindi chote hichi ambacho tumefanyakazi. *(Makofi)*

Napenda niwashukuruni sana kwamba pamoja na mivutano ya kawaida tu ya kibinadamu ya hapa na pale, basi kwa wale ambao walihisi walikwazana basi waweze kusameheana, ili mara nyengine tena tukija hapa tuweze kufanyakazi kwa mashirikiano ya hali ya juu kama ambavyo tumeanza na tumeanza kuzoea kwenda pamoja.

Waheshimiwa Wajumbe, pia naomba nitowe shukrani zangu za dhati sana kwa serikali, kwa shughuli zote ambazo zimewasilishwa na mashirikiano ambayo tumekuwanayo. Lakini pia niwashukuru na nyinyi kwa mashirikiano yenu nyinyi na serikali. Lakini pia nichukuwe nafasi hii kuwashukuru sana Mhe. Naibu wa Spika, pamoja na Wenyeviti kwa mashirikiano ambayo tumekuwanayo katika kusaidia kukiendesha chombo hiki. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo machache kwa heshima na taathima naomba sasa nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili sasa aje kuwasilisha hoja yake ya kuahirisha Baraza hili la Wawakilishi. Karibu sana Mhe. Makamu. *(Makofi)*

KUAHIRISHA BARAZA

Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mwingi wa Rehema kwa kuendelea kuiweka nchi yetu hii katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano mkubwa. Hali ambayo imeiwezesha serikali na wananchi kuendelea na shughuli zao za kila siku bila ya mtafaruku wa aina yoyote. Aidha, nawaomba wananchi waendeleo kuitunza na kuithamini amani iliopo nchini.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya njema na kutuwezesha kufanikisha vizuri Mkutano wa Tatu wa Baraza hili Tukufu la Tisa la Wawakilishi, ulioanza tarehe 21 Septemba, 2016. Nimefarijika kuwa kazi zote zilizopangwa katika ratiba yetu tumezikamilisha kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, napenda kutoa pongezi maalum kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kusimamia amani na utulivu hapa nchini pamoja na kutekeleza kwa vitendo na umahiri mkubwa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Mhe. Rais, amekuwa muhubiri mkubwa wa amani na utulivu wa nchi yetu. Amefanya hivyo kwa kujua kuwa amani ni chachu ya maendeleo, bila ya amani hakuna maendeleo. Nawaomba Wajumbe tuungane na Rais wetu katika kuhubiri amani katika majimbo yetu. Tuwalaani kwa nguvu zetu zote wale wote watakojaribu kufanya vitendo na vituko, vitakavyohatarisha uvunjifu wa amani na utulivu tulionao na tunaajivunia.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kutoa pole kwa familia, Serikali na Wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, kwa kifo cha aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa Awamu ya Pili na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Marehemu Alhaj Aboud Jumbe Mwinyi kilichotokea tarehe 14 Agosti, 2016 na kuzikwa tarehe 15 Agosti, 2016. Marehemu Mzee Jumbe atakumbukwa kwa michango yake mikubwa kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla hasa kwa kuimarisha demokrasia ikiwemo kutungwa kwa Katiba ya Zanzibar, kuanzisha Baraza la Wawakilishi pamoja na kuimarishwa mihimili mitatu ya dola, ndiyo maana leo tunafurahia demokrasia aliyotuachia kupitia chombo hiki tukufu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu Aboud Jumbe mahala pema peponi – *Amin*.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kufanikisha kwa wakati ahadi alizozitoa kwamba ifikapo tarehe 20 Septemba, 2016 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari itakuwa imeshanunua ndege mbili mpya. Ni ukweli usiopingika tayari ndege mbili aina *Bombardier Dash – 8 Q400* zimeshanunuliwa na kuwasili nchini Tanzania. Hii imeonyesha imani na upendo wa dhati alionao kwa wananchi wake wa Tanzania anaowaongoza. Pia, ndege hizi ni chachu ya kukuza uchumi wa Tanzania, na zitasaidia usafiri wa uhakika wa Watanzania. Nawaomba watakao kabidhiwa dhamana ya kuziendesha ndege hizi chini ya Shirika la Ndege la Tanzania (*ATCL*) waziendeshe ndege hizo vizuri pamoja na Shirika lenyewe, ili ziweze kutuhudumia kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, naomba pia kuchukua nafasi hii kuwapa pole wananchi wa Tanzania, Mkoa wa Kagera, kwa madhara waliyoyapata kutokana na tetemeko la ardhi, lilitokea tarehe 10 Septemba, mwaka huu lililosababisha vifo na majeruhi pamoja na kuathiri miundombinu na makaazi ya watu pamoja na sekta muhimu za kijamii. Ntoa shukrani za dhati kwa Watanzania wote waliopo ndani na nje ya Tanzania, pamoja na raia wengine wa nchi za nje wakiwemo wa nchi jirani kwa kuonesha imani kubwa kwa waliopatwa na maafa hayo kwa misaada yao ya hali na mali. Ntoa wito kwa wananchi wote wa ndani na nje ya Tanzania kuendelea kuchangia kwa hali na mali ili kurejesha hali ya mikoa iliyoathirika katika sura mpya.

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba mnamo tarehe 15 Februari, 2016 Serikali ilitoa uamuzi wa kuwahamisha wafanya biashara wa makontena Darajani na wale wa jengo la treni na kuwahamishia eneo la Saateni. Zoezi hilo lilifanyika kuanzia tarehe 15 Februari, 2016. Uamuzi huo umetokana na haja ya kubadilisha mandhari na haiba ya mji wetu na sio kuwakomoa wafanya biashara hao kama inavyodaiwa na baadhi ya watu wasioitakia mema Zanzibar.

Aidha, napenda kutoa taarifa kwamba zoezi hili ni endelevu ambalo litaendelea katika maeneo mengine ambayo wafanya biashara wameyavamia, na kufanya biashara zao bila ya mpango maalum. Serikali ina nia ya dhati ya kuuletea mji wa Zanzibar haiba inayostahili. Tunawaomba wananchi waliunge mkono zoezi hili. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nachukua fursa hii tena kwa niaba ya Baraza lako Tukufu, kutoa masikitiko yetu na pole zetu nyingi kwa wananchi wa Pemba waliokatiwa vipando vyao vya mikarafuu na miti ya matunda, pamoja na kubomolewa

nyumba zao bila ya sababu zozote za msingi. Tunakilaani kwa nguvu zetu zote kitendo hicho, kwani hakikuwa cha kiungwana wala ustaarabu bali kilikuwa kitendo cha kifisadi tu.

Mhe. Spika, katika kikao hiki jumla ya Maswali ya Msingi 74 na maswali ya nyongeza 181 yaliulizwa na yalijibiwa, naomba nichuku nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe, kwa kutumia nafasi yao ya kuihoji Serikali. Pia, natoa pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, kwa namna walivyoweza kuyajibu maswali hayo na kutoa ufafanuzi wa dhati. Nawapongeza sana Mawaziri hao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba nitoe shukurani na pongezi maalum kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa namna anavyosaidia katika kutoa ufafanuzi wa kisheria kila ilipojitokeza jambo ambalo lilihitajika, amefanya kazi kubwa nzuri na ameonyesha umahiri mkubwa katika fani yake ya sheria.

Mhe. Spika, miononi mwa mambo yaliyojitokeza katika mkutano huu ni harambee ya kuchangia pesa kwa ajili ya wananchi waliopatwa na maafa ya tetemeko katika Mkoa wa Kagera na mikoa ya jirani, baada ya kujadiliwa na baraza lako tukufu Waheshimiwa Wajumbe kwa pamoja walikubali kuchangia posho zao za siku moja kwa kila mjumbe wa Baraza lako tukufu, ili liwasilishwe katika mikoa iliyoapatwa na maafa na tetemeko. Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa namna ya uamuzi wao huo na wale wote waliofanikisha zoezi hili, michango hiyo ilionesha mshikamano mkubwa wa Watanzania kila maafa yanapotokea katika nchi yetu.

Mhe. Spika, aidha katika mkutano huu jumla ya miswada mitano imejadiliwa na kupitishwa kwa sheria na Baraza lako tukufu. Miswada yenyewe ni:

Mswada wa Sheria wa kuanzisha taasisi ya Elimu ya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar Nam. 8 ya 1999 kama ilivyorekebisha na Sheria Nam.11 ya mwaka 2019 na kuwekwa Masharti bora pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mswada wa Sheria za Marekebisha ya Sheria mbali mbali na kuweka Masharti yaliyobora kuhusiana na mambo hayo.

Mswada wa Sheria ya Mafuta, Utafiti na Uchimbaji na Gesi asilia.

Na mswada wa Tano Mswada wa Sheria wa kufanya marekebisho ya 11 ya Katiba ya Zanzibar inayohusu kifungu cha 66.

Kwa kupitishwa Mswada huu Rais kwa sasa ataweza kuzitumia nafasi zake 10 bila ya kuwepo kwa masharti magumu ya kikatiba na hasa kuhusiana na nafasi mbili kwa ajili ya upande wa Upinzani.

Mhe. Spika, Pamoja na Masuali hayo na Miswada hiyo, Baraza pia lilipokea maombi au *petition* kutoka kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Paje, kuhusu kuchukuliwa hatua za haraka za kuepusha usumbufu usiokuwa wa lazima kwa kupatikana kwa huduma mbali mbali za afya katika Taasisi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa sababu ombi hili lilielekezwa kwa Serikali, Serikali imepokea ombi hilo kwa utekelezaji.

Aidha, Baraza lilipokea hoja binafsi kutoka kwa Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae, kuhusu ukiukwaji wa Sheria kwa baadhi ya Taasisi ambazo zinatakuwa kuwasilisha taarifa zake mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa sheria, hoja hii nayo pamoja na maazimio yake ilipokelewa na Serikali kwa utekelezaji. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hata hivyo, napenda kuwapongeza sana Mawaziri waliotoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo yaliyokuwemo katika hoja hiyo, ni imani yangu kwamba Miswada hiyo mitano tuliyopitisha itasaidia kwa kuweka misingi bora ya utendaji na pia kukuza uchumi wa Zanzibar. Ni ukweli usipingika kwamba kupatikana kwa mafuta na gesi kutaiwezesha nchi yetu kukua kwa haraka kiuchumi, kwa kuiongezea mapato Serikali na wananchi kwa ujumla na pia kuongeza ajira kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, yote haya yataweza kufikiwa iwapo Sheria tulizozitunga katika Baraza hili zitashirikiana katika kuifanya kazi kama inavyotakiwa, hata hivyo napenda kutanabahisha kwamba tulichokuwa nacho hivi sasa ni Sheria na sio mafuta na gesi asilia, baada ya kukamilika kwa utafiti ndipo itajulikana kiwango gani cha mafuta na gesi asilia kilichopo nchini.

Mhe. Spika, kupitishwa kwa Mswada wa Mafuta na Gesi Asilia ni jambo la historia kwetu, hivyo, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein, amekubali kuiweka saina sheria hiyo mbele ya vyombo vya habari, pamoja na Kamati ya Katiba na Sheria ya Baraza la Wawakilishi na Kamati ya Uongozi ya Baraza la Wawakilishi ili wananchi washuhudie kitengo hicho. Nawaahidi Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe.

Spika, kuwa haitochukua muda mrefu kitendo hicho kitafanyika. Nawapongeza Wajumbe kwa kuipitisha miswada hiyo kwa kauli moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Serikali inatambua hofu waliyonayo baadhi ya wananchi juu ya mikataba inayohusiana na masuala ya mafuta na gesi asilia. Kwa kulitambua hilo Serikali imejipanga vyema kuwa na mikataba bora ambayo italeta tija kwa nchi yetu na watu wake, aidha, mikataba yote hiyo itakayohusiana na mafuta na gesi asilia itafanywa kwa uwazi, lengo ni kuwa uwazi ambao utaipatika heshima nchi yetu na kupunguza malalamiko na minong'ono isiyokuwa ya lazima.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru wale wote waliotuwezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu wa Tatu wa Baraza la Tisa la Wawakilishi kwa ufafanuzi mkubwa, pongezi hizo zaidi ziwafikie watendaji wote wa Baraza hili la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu Ndugu Raya Issa Mselem, ni ukweli usiofichika kwamba tumeanza vizuri na naamini tutaendelea vizuri. Mungu libariki Baraza lako hili. Mungu ibariki Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

Pia, nawapongeza wakalimani wetu wa lugha za alama ambao wamewawezesha Waheshimiwa Wawakilishi, wenye ulemavu wa kusikia kufuatilia yote yaliyokuwa yakiendelea ndani ya Baraza hili, vile vile, nawashukuru wanahabari kwa kufanya kazi ya kuhabarisha wananchi wetu yale yaliyokuwa yakiendelea ndani ya Baraza hili.

Mwisho, Mhe. Spika, nikupongeze wewe binafsi, nimpongeze Mhe. Naibu Spika, na Wenyeviti wa Baraza kwa kuliongoza vizuri na kwa ufanisi mkubwa wa Baraza hili, hekima na busara zenu zimesaidia sana katika kumaliza mkutano huu salama.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nawatakia Waheshimiwa Wawakilishi, kila la kheri na mafanikio mema katika kuwatumikia wananchi wao Majimboni mwao, aidha, nawatakia safari njema na salama ya kurudi majimboni mwao na hasa wawakilishi wenzetu kutoka Pemba ukomavu wao uwe wa safari ndefu zaidi kuliko wenzao wa Unguja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kwa heshima na taadhima kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liakhirishwe hadi siku ya Jumatano tarehe 23 Novemba, 2016 saa 3.00 za asubuhi panapo majaaliwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Ahsanteni sana Waheshimiwa, ahsante sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa hoja hiyo ambayo umeittoa. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa napenda nichukue nafasi hii kuwahoji, wale wote wanaounga mkono hoja kwamba tuakhirishe Kikao mpaka tarehe 23, Novemba, 2016, wanyanyue mikono yao, wanaokataa. waliokubali wameshinda (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaakhirisha labda nitoe matangazo machache. Kwanza kabisa kabla sijatangazia naomba nitoe shukurani zangu za dhati sana kwa Waheshimiwa Waandishi wa habari ambao tumeshirikiana muda wote, najua tumekuwa pamoja hapa katika kufanya hizi shughuli pamoja na mashirikiano ambayo tumeyapata kutoka kwa Waheshimiwa.

Sasa baada ya hayo, naomba nikupeni matangazo machache Waheshimiwa, kwanza kabisa Waheshimiwa wote mnaarifiwa kwamba kutakuwa na mechi kati ya Timu ya Wawakilishi *Sport Club* na *NMB Bank* itakayofanyika siku ya Jumamosi tarehe 8/10/2016 katika uwanja wa Amani saa 10.00 jioni.

Pia, mnaarifiwa Waheshimiwa, Mazoezi yataanza siku ya Jumatano tarehe 5/10/2016 saa .12.00 asubuhi katika uwanja wa Mao, yote hayo ni maandalizi ya michezo kati ya Wawakilishi *Sport Club* na Timu ya Wabunge *Sport Club* hapo baadae Mjini Dodoma. Taarifa hii nimeletewa na Katibu Msaidizi wa Wawakilishi *Sport Club* Mhe. Ali Salum Haji.

Naakhirisha Kikao hichi mpaka Jumatano tarehe 23, Novemba. 2016 saa 3.00 asubuhi.

(Saa 12.09 jioni Baraza liliahirishwa hadi tarehe 23 Novemba, 2016 saa 3.00 asubuhi)